**SERIKALI** na wafanyabiashara watoka na maazimio 15 kumaliza mgomo
UKURASA 2

**BITEKO** asema utamaduni wa kigeni unaumiza taifa kwa mengi
UKURASA 3



**UNDANI** wa kinachojiri vurugu vijana wa GZ Kenya
UKURASA 19

ISSN 0856 • No. 0581721
Ijumaa Juni 28, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**KIVUMBI 16 BORA EURO 2024**
UKURASA 22



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, picha nyuma ni Mbunge Jesca Msambatavangu

## UFADHILI BIMA YA AFYA

# Vilevi, vipodozi na kubeti vyapingwa

**MBUNGE** acharuka ni haramu... *Endelea ukurasa 2*

# Prof. Janabi aibukia Kliniki ya Makonda

**ATAJA** mzizi upungufu nguvu za kiume *Uk. 5*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikata utepe kuzindua Bohari ya Kwanza ya Kupokea na Kuhifadhia Gesi ya Kampuni ya Oryx Gas Zanzibar, eneo la Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Vigor, Toufiq Salim Turky (kushoto kwa Rais), Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Oryx Gas, Benoit Araman (wa tatu kulia), Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar, Zena Ahmed Said (kulia), Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Shaib Kaduara (wa tatu kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Rashid Hadid Rashid (wa pili kushoto) na Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi CCM Zanzibar, Khamis Mbeto. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**




UKURASA WA 5

## UCHUNGUZI WAANZA UDHALILISHAJI KATIKA MIKOPO MTANDAONI

VILEVILE, imetoa ufafanuzi kuhusu mikopo ambayo baadhi ya wakopaji wamekuwa wakidhalilishwa pale wanaposhindwa...

## Safari za ATCL sasa rasmi Oman

UKURASA 3

**MICHEZO** **SEKILOJO ASHAURI MAMBO 4 YANGA** UK 24

**MAONI, KATUNI UK.6**



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiangalia madini ya makaa ya mawe yanayochimbwa huko mgodi wa Liganga, Wilaya ya Ludewa, mkoani Njombe, alipotembelea banda la madini la mkoa huo, kwenye kilele cha maonyesho ya Wiki ya Madini 2024 jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali, wafanyabiashara watoka na maazimio 15 kumaliza mgomo

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI na Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania wamekubaliana mambo 15 ya kutekelezwa katika kushughulikia malalamiko ya kundi hilo lililoitisha mgomo kwa simu nne sasa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana kuhusu maazimio ya kikao cha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na wawakilishi hao wa wafanyabiashara, Msemaji Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo, Thobias Makoba, alisema mazungumzo hayo yalitokana na madai na hoja takribani 41 zilizowasilishwa.

"Kutokana na hoja hizo, na baada ya vikao na mawaziri wa sekta husika, Waziri Mkuu kwa kutumia falsafa ya R4 za Rais Samia Suluhu Hassan, amehitimisha mazungumzo hayo, wameafikiana kusimamia maazimio 15 ambayo ndani yake serikali imetoa maagizo," alisema.

Makoba alitaja maazimio hayo kuwa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kusitisha mara moja mazoezi yote ya kamatakamata pamoja na kusitisha mazoezi mengine yote ya ufuatiliaji risiti za kielektroniki (EFD) katika maeneo yote nchini hadi Agosti mwaka huu, na kwamba wafanyabiashara wanahimizwa kuendelea kutoa risiti za mauzo.

Lingine ni TRA kuweka mfumo mzuri utakaowezesha utoaji nyaraka muhimu za ununuzi wakati wa uingizaji bidhaa nchini kuanzia Julai, mwaka huu na kwamba utekelezaji wake utawekewa utaratibu mzuri kwa kushirikisha wadau wote.

Serikali pia imeagiza Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kuongeza haraka Bandari Kavu (ICD) kwa ajili ya kurahisisha utoaji mizigo kupitia utaratibu wa deconsolidation.

Alisema azimio lingine ni TRA kuongeza nguvu kwenye kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kodi na maboresho ya kodi yanayofanyika ili kuwezesha kuongeza uelewa kwa wafanyabiashara kuhusu masuala ya kodi nchini. Taasisi husika za serikali pamoja na mabaraza ya biashara yashirikishwe kikamilifu katika ngazi zote.

Msemaji huyo alisema TRA pia inaelekezwa kubainisha na kusimamia vyema orodha ya bidhaa nane ambazo zitawekewa bei elekezi kama ilivyo katika bidhaa za magari yalivyotumika. Bidhaa hizo ni vitenge, mashati, nguo nyingine, vipodozi, vito vya thamani, nguo za ndani, leso na vesti.

Makoba alisema serikali kwa ujumla itaendelea na zoezi la kuwapanga na kuwawekea mazingira rafiki wafanyabiashara wadogo ambao hawako kwenye maeneo rasmi ili kurahisisha usimamizi, ufuatiliaji na urasimishaji wao wa biashara.

Alisema katika kipindi cha muda wa kati, serikali itaendelea kufanya mapitio ya viwango vya kodi ilivyo navyo kwa sasa ili kuwawezesha wafanyabiashara kulipa kodi kwa amani na haki kulingana na thamani ya biashara zao.

Makoba alisema kuwa katika kipindi cha muda mfupi na wa kati, serikali itashughulikia changamoto zote za wafanyabiashara zilizowasilishwa serikalini hususan zile ambazo zinahitaji mabadiliko ya sera au sheria.

Vilevile, katika maboresho zaidi, serikali imeagiza TRA ikamilishe maboresho ya mfumo wa TANCIS ambao utajumuisha moduli ya Auto valuation itakayoweka uwazi na usawa katika ukokotoaji kodi kufikia Januari 2025.

Azimio lingine ni wataalamu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na TRA kwa pamoja wakamilishe marekebisho ya mfumo wa TEHAMA, ili mizigo inayoingia nchini kwa njia ya uchangiaji makasha igombolewe kwa namba ya usajili wa mlipakodi (TIN) ya mwenye mzigo badala ya TIN ya wakala bila ya kuwa na gharama za ziada kwa mlipakodi. Zoezi hili linatarajiwa kukamilika mwezi ujao.

Serikali pia imeelekeza Wizara ya Fedha kuratibu uchambuzi, tathmini na mapitio ya mfumo mzima wa utozaji na ukusanyaji pamoja na viwango vya Ushuru wa Huduma (Service Levy) pamoja na kushauri njia mbadala ya utozaji itakayokuwa rafiki zaidi kwa wafanyabiashara ili kulinda mitaji na ukuaji wa biashara nchini.

Kuhusu wafanyabiashara kutoka nje ya nchi, Msemaji huyo alisema serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) na mamlaka zingine husika, itaendelea kuimarisha ukaguzi wa vibali vya kazi kwa wageni ili kuhakikisha wamiliki wa vibali hivyo wanafuata masharti ya vibali hivyo kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wanaokiuka sheria, kanuni, taratibu na masharti ya vibali vya ajira ikiwa ni pamoja na kuwafukuza nchini na waajiri husika kuchukuliwa hatua za kisheria.

Msemaji huyo alisema azimio lingine ni mawaziri wanaohusika na sekta ya biashara watakutana na wafanyabiashara wote nchini kwa ajili ya kusikiliza changamoto za wafanyabiashara pamoja na kupokea maoni yatakayolenga kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara nchini wakati wote.

Pia wamekubaliana wataalamu wa forodha wakutane na Jumuiya ya Wafanyabishara nchini mara moja ili kujadiliana kuhusu taratibu za forodha husani uthaminishaji na ugomboaji mizigo na kwamba suala hilo linapaswa kukamilika Julai 10, mwaka huu.

Azimio lingine ni Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) iendelee kuratibu suala la kutoa mrejesho kwa wafanyabiashara kila robo mwaka kuhusu utekelezaji maazimio baina ya wafanyabiashara na serikali.

"Kutokana na maazimio haya na maagizo ya serikali, pande zote mbili zimekubaliana hali ya biashara kote nchini kuendelea kama kawaida ili kuwapa Watanzania huduma wanazostahili. Kwa maslahi mapana ya nchi yetu, serikali itaendelea kuboresha mazingira ya wafanyabiashara wote kama ambavyo Rais amekuwa akisisitiza katika uongozi wake," alisema.

# Vilevi, vipodozi na kubeti vyapingwa kufadhili bima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MBUNGE wa Iringa Mjini, Jesca Msambatavangu (CCM) amesema hakubaliani na Wizara ya Fedha kupendekeza vinywaji baridi, pombe kali, vipodozi pamoja na kamari kutumika kama vyanzo vya mapato kwa ajili ya kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote.

Jesca alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akichangia mjadala wa muswada wa Fedha wa mwaka 2024 ulisomwa kwa mara ya pili na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba.

Alisema si jambo zuri kwa kinamama wajawazito na watoto kupatiwa matibabu yao kwa fedha zitokanazo na walevi, hivyo serikali inapaswa kutafuta chanzo kingine cha uhakika.

"Haiwezekani leo hii tutegemee pombe, sigara, soda na vipodozi kwa ajili ya kuhudumia matibabu ya watoto wetu, wazee wetu watibiwe kwa fedha za walevi kweli au wachezakamari, hii haiwezekani!

"Chanzo hiki si 'reliable' (cha kuaminika) viongozi tafuteni chanzo kingine. Kweli leo hii Bima ya Afya kutegemea fedha za walevi au kinamama wanaojipodoa, si kweli!" Jesca alilalama.

Kutokana na hoja hiyo, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu, alisimama na kuomba kutoa taarifa, alipopata rukhsa ya Spika, alisema lengo la serikali kutoza kodi kwa bidhaa hizo ni kupunguza matumizi ya bidhaa hizo kwa wananchi wake.

"Mheshimiwa Spika, viwango vya hizi bima za afya katika maeneo mengi vinatokana na tozo za kodi za bidhaa hizi ambazo zinahatarisha afya za watumiaji ili kiasi kile kinachotozwa kinakwenda kutibu watu," alisema waziri huyo.

Baada ya Dk. Mwigulu kutoa taarifa hiyo, Spika Dk. Tulia Ackson alimwuliza mbunge huyo kama anapokea taarifa hiyo; naye alisema anaipokea lakini akasisitiza serikali itafute chanzo kingine chenye uhakika kwa ajili ya kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote.

"Ninaipokea taarifa lakini kama alivyosema, wanatoza kodi ili kupunguza matumizi ya bidhaa hizo na kama kweli watu hawatatumia, maana yake fedha hazitakuwapo kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote. Kwahiyo, chanzo hiki kimewekwa tu lakini pia sisi kutumia fedha za walevi kutibiwa haileti picha nzuri," alisema.

**KODI YA GESI**

Naye Mbunge wa Kalambo, Josephat Kandege (CCM), akichangia mjadala huo, alisema mpango wa serikali kutoza Sh. 382 kwa kilo moja ya gesi asilia unarudisha nyuma jitihada za nchi kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi.

Kandege alisema matumizi ya gesi asilia yatakuwa na manufaa kwa taifa, hivyo kuweka ushuru huo ni kurudisha nyuma jitihada za serikali. "Gesi asilia ambayo tutahamasisha wananchi watumie, tunainunua kwa shilingi yetu, hivyo tutaokoa matumizi ya fedha za kigeni ambazo tunatumia hivi sasa kuagiza mafuta nje ya nchi," alisema Kandege.

Mbunge huyo pia alishauri magari yote ya serikali ambayo yananunuliwa yawe na mifumo miwili ya matumizi ya mafuta na gesi, ili kuhamasisha matumizi hayo na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza mafuta.

HABARI KITAIFA

# Biteko ataja chanzo mmomonyoko maadili

Na Jenifer Gilla

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko amesema vitendo vya mmomonyoko wa maadili vinavyotokea nchini ikiwamo mauaji ya watu wenye ualbino na mapenzi ya jinsia moja ni matokeo ya Watanzania kuuacha utamaduni wao na kuukumbatia wa mataifa mengine. Biteko aliyasema hayo jana katika Tamasha la Utamaduni la Bulabo 2024 lililofanyika katika Kata ya Kisesa, Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza, lenye kaulimbiu "Tudumishe Mila na Tamaduni zetu, Tushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024".

Alisema anashangazwa na baadhi ya Watanzania kuyafanya mauaji ya watu wenye ualbino kama sehemu ya utamaduni wao, akisema kuwa imetokana baadhi ya watu kuchukua utamaduni wa mataifa mengine.

"Wakati fulani unajiuliza hivi inakuwaje, mauaji ya watu wenye ualbino yanafanywa kuwa ni utamaduni kwa baadhi ya watu, unajiuliza mapenzi na ndoa za jinsia moja kwa nini zije miongoni mwetu? Ni kwa sababu tumechukua tamaduni za watu wengine na kuzileta miongoni mwetu," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kuyatumia matamasha hayo kujikumbusha umuhimu wa utamaduni wao, kuenzi na kuziishi mila na desturi zao, kinyume na hapo watakuwa taifa lisilokuwa na utambulisho na kupokea kila wanacholetewa.

Aliipongeza jamii ya Wasukuma kwa kuendelea kuenzi, kuheshimu na utamaduni wake licha ya kukua kwa sayansi na teknolojia. Aliiagiza Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuunga mkono jamii zote zinazoenzi tamaduni zao.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kama mmoja wa machifu nchini anatambua umuhimu wa tamasha hilo na ndio maana serikali inaunga mkono wakati wote.

Alisema Rais alimwagiza pamoja na mambo mengine awaelekeze mikoa yote ya Kanda ya Ziwa washirikiane kwa karibu ili tamasha hilo liwe pana zaidi na kuzielekeza sekretarieti za mikoa na halmashauri zote kutenga bajeti kwa ajili ya kusaidia shughuli muhimu za kuendeleza urithi na utamaduni wa sanaa ili vipewe kipaumbele.

Alisema Rais pia ameiagiza Wizara ya Utamaduni, Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), ziboreshe mashindano ya michezo, sanaa na taaluma kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na kujumuisha midahalo ya maadili, ili wanaoshiriki wafundishwe umuhimu wa kuenzi utamaduni wao.

Aidha, Biteko aliwakumbusha Watanzania kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba, mwaka huu na kuwachagua viongozi wa kuzingatia uwezo wao wa kuwaletea maendeleo na si fedha. Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbalo, alisema tamasha hilo ni la kipekee nchini kwa sababu limeenzi utamaduni kwa miaka 56, linafungamanisha utamaduni wa Mwafrika na dini ya kikristo na kuunganisha mikoa yote ya Kanda ya Ziwa.

Alisema mwaka huu Tamasha la Kitaifa litafanyika Songea na kuwaalika Watanzania wote kuhudhuria. Pia wamejipanga kulifanya kuwa la kimataifa kuanzia mwakani kwa kuwashirikisha wadau kutoka maeneo mbalimbali.

## ATCL sasa kwenda Oman

Na Joseph Mwendapole

KATIKA kutanua wigo wa safari zake za kimataifa, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), iko kwenye maandalizi ya kuanzisha safari za moja kwa moja kuelekea Muscat nchini Oman.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Mhandisi Ladislaus Matindi, alipokutana na Balozi wa Oman nchini, Saud bin Hilal Alshaidani, juzi katika Ofisi za Ubalozi zilizopo jijini Dar es Salaam.

"Taratibu za kufungua kituo nchini Oman zimeanza ambapo Air Tanzania tumeshampata wakala mkuu wa mauzo ya tiketi zake nchini Oman (General Sales Agent), tumeteua msimamizi wa kituo hicho," alisema Mhandisi Matindi.

Aliongeza kuwa kwa sasa hatua iliyofikiwa ni kukamilisha uandaaji wa timu ya marubani, ndege itakayotumika pamoja mpangilio wa safari.

Balozi wa Oman nchini Tanzania, Saud bin Hilal Alshaidani, alisema mazungumzo yake na Air Tanzania yamekuwa na tija na wamejadili fursa zilizopo kwa kutumia ndege za abiria na mizigo.

"Kwa idadi kubwa ya raia wa Oman waliopo hapa nchini, biashara kati ya nchi hizi mbili ikiendelea kukua ni matarajio yangu kuwa Air Tanzania itanufaika na fursa hii bila kuwa na mshindani," alisema Balozi Alshaidani.

"Tunaweza kujikita kwenye usafirishaji wa aina tatu za matunda zenye uhitaji mkubwa nchini Oman, maembe, nanasi na parachichi. Hii itanufaisha pande zote, wafanyabiashara wa Tanzania na Oman," alisema.

Kwa sasa Air Tanzania inafanya safari za ndani ya nchi kwa zaidi ya vituo 10. Kwa safari za kikanda na kimataifa ina safari za Dubai (UAE), Mumbai (India), Guangzhou (China), Bujumbura (Burundi), Entebbe (Uganda), Hahaya (Comoro), Harare (Zimbabwe), Lusaka na Ndola (Zambia), Nairobi (Kenya) na Lubumbashi (Congo).

Kwa Tanzania ATCL imekuwa ikifanya safari zake kati ya Dar es Salaam kwenda mikoa ya Dodoma, Mwanza, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha, Songea, Katavi, Zanzibar, Mtwara, Tabora na Kigoma.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Mchengerwa awapa somo ma-RC kupitia Makonda

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa amesema anaridhishwa na utendaji kazi wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda na kuwataka wengine kuiga mfano na kuwa wabunifu katika kutatua kero za wananchi.

Alitoa kauli hiyo jijini jana wakati wa uzinduzi wa Programu ya Uimarishaji wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo inatekelezwa kwa kipindi cha miaka 10 kwa gharama ya Sh. bilioni 400.

Mchengerwa alisema, "Nipende kuweka wazi -ninafurahishwa na utendaji wa Mkuu wa Mkoa wa Arusha (Makonda), hilo bila kuficha nimesema ukweli, ninaomba (mwakilishi) fikisha salamu hizo."

Mchengerwa aliwataka wakuu wa mikoa na watendaji wengine wa mamlaka za serikali za mitaa nchini kuhakikisha wanaongeza kasi ya usikilizaji kero za wananchi na kuzitatua.

"Nchi hii ni ya wananchi, hakuna namna, niliwaambia ukiwa mkuu wa mkoa au kiongozi ndani ya serikali, ukijishusha cheo chako hakiwezi kuondoka, kitabaki palepale, lakini tutaendelea kuongeza imani kwa wananchi na kulinda na kuongeza kura.

"Tunatambua yapo maeneo wasaidizi wetu hawajatuelewa vizuri, hatuna budi kuwasaidia ili waweze kutuelewa maana kuna wengine wanahisi masuala mengine si yao, mfano miradi, hivyo hii lazima tukairekebishe," alisema.

Waziri Mchengerwa alisema kuwa kila mkuu wa mkoa ana hulka ya utendaji kazi.

Hata hivyo, serikali inataka kuona kero zikitatuliwa moja kwa moja kwa wananchi kule chini na kuwe na utendaji wa ubunifu ili kupunguza malalamiko kwa wananchi.

Kuhusu programu hiyo, waziri huyo alisema inalenga kuamsha chachu ya utendaji kazi katika maeneo yao ya utawala.

"Rais ametuletea programu hii ili tuboreshe maeneo ya utendaji kazi wetu, kazi tuliyobaki nayo ni utoaji huduma na kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja," alisema.

Waziri huyo alisema uanishwaji wake ni mwendelezo wa juhudi za serikali kupanua wigo wa ugatuaji madaraka kwa wananchi kwa kuimarisha Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Ndege ya ATCL, Mhandisi Ladislaus Matindi (kushoto), akikabidhi jarida la Twiga la ndani ya ndege za shirika hilo, kwa Balozi wa Oman nchini, Saud bin Hilal Alshaidani, walipokutana kwa mazungumzo kwenye Ofisi za Ubalozi huo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Majaliwa ataka mipango endelevu utafutaji teknolojia sekta ya madini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza Wizara ya Madini iendelee kushirikiana na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika kutafuta teknolojia mbalimbali za uongezaji thamani madini.

Amesema kwa kufanya hivyo kutawezesha madini yanayopatikana nchini kutumika katika kuzalisha bidhaa ambazo zinahitajika duniani kote kutokana na kuongezeka mahitaji, pia ongezeko la idadi ya watu duniani.

Majaliwa alitoa maagizo hayo jana wakati akifunga Wiki ya Madini iliyoambatana na Kongamano la Wachimbaji Madini, Mkutano Mkuu wa FEMATA na Maonesho ya Madini na Vifaa vya Uchimbaji iliyofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, jijini Dodoma.

Alitoa rai kwa wafanyabiashara, taasisi za elimu, fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Madini kuendelea kuweka mikakati ya kuwezesha uwekezaji wa ndani wa teknolojia mbalimbali zitakazowezesha upatikanaji malighafi zinazohitajika na migodi na shughuli nyingine za madini.

"Kwa kuwa teknolojia duniani inazidi kukua kwa kasi, wadau wa madini waongeze na kuimarisha mtandao na wachimbaji wa kikanda na kimataifa.

"Kwa kujifungia ndani peke yetu hatutapata suluhisho la changamoto tulizonazo bali tutachelewesha maendeleo yetu," alionya.

Waziri Mkuu alisema serikali itaendelea kutatua changamoto, kero na adha zinazokabili wawekezaji na wachimbaji wa madini pamoja na kuhakikisha wanapata masoko ya uhakika ya kuuza madini pamoja na kuendelea kuwezesha wawekezaji wadogo katika Sekta ya Madini kwa kuwaunganisha na taasisi za fedha nchini ili wapewe mikopo.

"Katika hili nitoe wito kwa taasisi za fedha nchini kukaa na FEMATA, wapeni miongozo na elimu ya mitaji ili waweze kuitumia katika kuzipa thamani kazi zao ili ziwe na tija," aliagiza.

Waziri Mkuu, akiwa katika banda la kampuni wezeshi ya mitambo ya kuchimba madini ya BigBang Shantui, aliipongeza kwa kutoa mikopo ya mitambo kwa wachimbaji wadogo ili kuwarahisishia shughuli za uchimbaji nchini.

Meneja Biashara ya Mashine wa kampuni hiyo, Glenn Malya alisema wana mpango mkakati wa kukopesha mitambo ya uchimbaji madini kwa wachimbaji wadogo nchini kwa ushirikiano na benki ambapo mchimbaji hutoa asilimia 20 ya gharama yote.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuipa nguvu sekta ya madini ili iendelee kutoa mchango katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania

Alisema serikali imeongeza bajeti ya Wizara ya Madini kutoka Sh. bilioni 89 hadi kufikia Sh. bilioni 231.

Rais wa Chama cha Wachimbaji Wadogo Tanzania (FEMATA), John Wambura amesema Tanzania ina fursa ya kuwa na Soko la Madini Afika kwa kuwa ina kila sifa ya kufikia hapo kutokana na juhudi zilizofanywa na Rais Samia.





Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Kasilda Mgeni, akizungumza katika mkutano wa hadhara wa kutatua kero za wananchi katika Kata ya Mamba Miyamba, wilayani humo juzi. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Prof. Janabi aibukia Kliniki ya Makonda

## -Ataja mzizi upungufu nguvu za kiume

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, amesema wananchi wa Mkoa wa Arusha wanaongoza kuwa na shinikizo la damu kwa kiwango kikubwa cha 180 kwa 110 kutokana na matumizi ya chumvi nyingi katika ulaji wa nyama.

Vilevile, watoto 10 wamebainika kuwa na korodani zinazopanda badala ya kushuka chini, hivyo watasafirishwa kupelekwa MNH kwa ajili ya upasuaji na gharama zake zitabebwa na serikali.

Prof. Janabi aliyasema hayo jana wakati akitoa elimu kwa wananchi waliojitokeza katika kambi maalum ya siku saba ya utoaji huduma za afya bila ghrama kwa wananchi jijini Arusha.

"Hisia yangu kubwa wanatumia chumvi nyingi kwenye nyama. Presha za Arusha zinatia wasiwasi kama tusipochukua hatua za makusudi matatizo ya magonjwa ya moyo, kiharusi na figo yatakuwa ni makubwa katika huu mkoa," alisema Prof. Janabi.

Mtaalamu huyo wa maradhi ya moyo alisema kwa wagonjwa aliohudumia jana, wamebainika kuwa na kiwango kikubwa cha shinikizo la damu, jambo ambalo linahatarisha afya zao kwa kuwa wanaweza kupata magonjwa.

"Wagonjwa wengi wamekutwa na shinikizo la juu la damu, ni muhimu mwelewe kuwa duniani kwa sasa kuna karibu watu bilioni 1.2 wana matatizo ya presha na asilimia 32 ya vifo vyote vinavyotokea duniani ni vya magonjwa ya moyo ambayo yanawekwa katika magonjwa yasiyoambukizwa," alisema.

Prof. Janabi alisema changamoto kubwa ya ugonjwa wa shinikizo la damu ni kukosa dalili, akifafanua"

**"Ninajua kwenye mitandao wanafanya dhihaka kidogo, bahati mbaya siku wakianza kuugua watu wa mitandaoni hawatakuwapo. Ninasisitiza kuwa pombe haijawahi kumwacha mtu salama. Tuwe waangalifu, tunywe kwa wastani."**

"Nimemsikia mgonjwa mmoja anasema ana presha, kichwa kinamuuma. Ninaomba nilisemee hivi; ukiwa na ugonjwa wa homa ya matumbo (typhoid) kichwa kitauma, ukiwa na U.T.I (maambukizi katika njia ya haja ndogop) kichwa kitauma na ukiwa na njaa kichwa kinauma, maana yake si dalili ya ugonjwa mmoja wa presha."

Alisema idadi ya watu wanaougua kiharusi inaongezeka kwa kasi kutokana na watu wengi kuwa na tatizo la shinikizo la damu; wanatembea na tatizo hilo bila wao kujua.

"Presha tunaita ni ni muuaji wa kimyakimya, anaua taratibu, wakati wagonjwa wanakwenda hospitalini wanakuwa wamechelewa kwa sababu unakuta presha imekaa kwa muda wa zaidi ya miaka mitano au kumi na kuharibu figo taratibu, kupanua moyo, kuharibu macho na inapunguza nguvu za kiume.

"Vijana wengi kwa sasa hivi wana tatizo kubwa la kuwa na nguvu kidogo za kiume na kinamama tendo la ndoa hamu ipo chini kwa sababu ya shinikizo la damu, siku wanayokwenda hospitalini, si tena tatizo la presha, unakutwa na tatizo la figo na magonjwa mengine," alisema Prof. Janabi.

Alisema MNH inasafisha figo kwa siku wagonjwa 150, asilimia 90 ya wagonjwa hao ni tatizo la shinikizo la damu na kusababisha figo zao kuharibika au kisukari.

Prof. Janabi alisema kwa changamoto aliyoona, kuna haja elimu kutolewa kwa umma, akisisitiza kuwa unaweza kuepuka magonjwa hayo kwa kutunza afya, ukizingatia uzito, lishe bora, mazoezi na kuchunguza afya walau mara mbili kwa mwaka kwa kuwa kinga ni rahisi kuliko tiba.

Alisema kuna watoto wana matatizo ya sukari na shinikizo la damu kutokana na vyakula wanavyokula.

Prof. Janabi alisema kwa wanyaji wa pombe, wanatakiwa kuzingatia kwa wanawake chupa moja na kinababa chupa mbili kwa kufuata masharti ya saa moja kwa bia moja.

"Ninajua kwenye mitandao wanafanya dhihaka kidogo, bahati mbaya siku wakianza kuugua watu wa mitandaoni hawatakuwapo. Ninasisitiza kuwa pombe haijawahi kumwacha mtu salama. Tuwe waangalifu, tunywe kwa wastani," alisema Prof. Janabi.

Aliongeza: Hawa watoto 10 ambao mbegu zao hazishuki, kuna uwezekano wakashindwa kuzalisha watoto wanapokuwa wakubwa, hivyo watapelekwa MNH kwa ajili upasuaji."

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alisema wameongeza mahema ili kupunguza foleni huku wakiongeza pia madaktari na wauguzi kufikia 550 kutoka 450 wa awali.

# Serikali yachunguza udhalilishaji kwenye mikopo ya mtandaoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaendelea na utafiti wa uanzishwaji matumizi ya sarafu za kidijitali za benki kuu (Central Bank Digital Currency).

Vilevile, imetoa ufafanuzi kuhusu mikopo mitandaoni ambayo baadhi ya wakopaji wamekuwa wakidhalilishwa pale wanaposhindwa kurejesha mikopo kwa wakati; watu wao wa karibu kutumiwa ujumbe kuhusu mkopo husika.

Naibu Waziri wa Fedha, Ahmad Chande, alizungumzia mchakato wa sarafu hiyo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Kigamboni, Dk. Faustine Ndungulile (CCM) aliyetaka kujua mpango wa serikali kuanza matumizi ya sarafu za kidijitali.

Chande alisema BoT imebaini kwamba, kama ilivyo kwa mataifa mengi, uanzishwaji sarafu za kidijitali za benki kuu unahitaji uangalifu na umakini bila kuleta athari hasi katika mifumo ya malipo nchini.

"Na pia kuweza kutatua tatizo halisi la malipo ambapo kwa sasa mifumo iliyopo nchini inakidhi hali halisi ya uwezeshaji mwananchi kutuma fedha na kufanya malipo," alisema.

Alisema soko la nchi bado linahitaji kuendelea kuboreshwa katika kuimarisha mifumo iliyopo kwa kutumia vyanzo vinavyopatikana kwa urahisi na wananchi wengi (simu za kawaida) tofauti na matumizi ya sarafu za kidijitali zinazohitaji matumizi ya simu janja.

"Nchi nyingi ikiwa ni pamoja na majirani zetu na ukanda wetu bado wapo katika hatua hizi za awali za utafiti na kuboresha mifumo ya malipo iliyopo," alisema Chande.

MIKOPO MTANDAONI

Kutokana na majibu hayo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitaka kupata ufafanuzi kuhusu kile kinachoendelea mitaani kuhusu mikopo inayotolewa kwa njia ya mtandao na watu kudhalilishwa.

"Sijui kuna mwongozo wowote ama na serikali mmepokea, mnalifanyia kazi ama hilo limekuwaje, maana hata mimi nimepata ujumbe wa mtu akiambiwa sijui anadaiwa.

"Sasa ninawaza mimi ninahusika vipi kwa yeye kudaiwa? Sasa ninaona limelalamikiwa sana na wananchi, sijui mna maelekezo yoyote upande wenu serikali kwa sababu hapa tunazungumzia hayohayo ya fedha za mitandao?" Spika Tulia alihoji.

Ni hoja iliyomwinua Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, aliyethibitisha kumekuwa na changamoto hiyo.

"Kuna watu ambao wanakopeshana mitandaoni, lakini baadaye wanatumia taarifa za watu wanaomzunguka yule waliyemkopesha kwa maana ya namba za simu na kuanza kumtisha pale ambapo wameshindwa kurudishiwa mkopo wao.

"Hili jambo limetokea kwa wiki kadhaa kama si miezi miwili mitatu na baada ya kuliona tumeagiza wenzetu wa TCRA (Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano nchini), wakishirikiana na Cyber Crime Unit ya Jeshi la Polisi, wanalifanyia kazi.

"Ni matumaini yangu kwamba hii kazi itakamilika mapema ili tuone msingi wa hili jambo, ukubwa wake na wapi wanapozipata hizi namba," alisema.

Nape aliongeza kuwa jambo hilo si la kiungwana na ni kinyume cha sheria na hasa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; kutumia taarifa za watu wengine kufanya chochote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upimaji mara kwa mara utapunguza tatizo kiafya

**UTARATIBU** wa kuanzisha kambi maalumu zinazosaidia wananchi wasioweza kumudu gharama, kupima afya umesaidia kugundua magonjwa mengi na kutoa fursa ya kusaidiwa matibabu.

Utaratibu huu umesaidia wananchi wengi kugundua maradhi ambayo walikuwa hawajui kama wanayo na hatimaye kupatiwa tiba.

Wakati Waziri wa Afya akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya bajeti ya wizara yake bungeni, alisema serikali inakusudia kuja na chombo muhimu kitakachokuwa kinadhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi.

Afya ni muhimu katika maisha ya binadamu hivyo ni lazima suala la gharama liangaliwe ili lisiwaumize wananchi hasa wasiokuwa na uwezo.

Kwa kuanzishwa chombo chenye uwezo wa kusimamia na kudhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi hususan wasio na bima ya afya, malalamiko yatapungua.

Utaratibu huu utasaidia kudhibiti utozaji gharama holela unaofanywa na baadhi ya madaktari katika hospitali za binafsi na zile za serikali ili kuwapa unafuu wananchi.

Vyombo kama hivi vimefanikiwa pia katika huduma za mafuta ya petroli ambapo inafahamika kila mtu anapokwenda kwenye kituo cha mafuta kujaza kwenye gari yake anakuta bei elekezi.

Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wagonjwa wanapokwenda kutibiwa kukuta wakitozwa gharama kubwa kumuona daktari kabla ya kupata matibabu, hali inayowafanya wasiokuwa na bima za afya kushindwa kulipia na kuamua kwenda kujaribu tiba zingine mbadala.

Kwa mujibu wa wasilisho la makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Fedha, kwenye vitita vya NHIF, madaktari bingwa katika ngazi ya rufani mkoa, ada imeongezeka kutoka Sh. 15,000 hadi 25,000 ambayo ni sawa na kumuona daktari aliyepo ngazi ya kanda na taifa.

Kiwango hiki cha kumwona daktari kinatoa hamasa kwa madaktari hao kufanya kazi katika mazingira yoyote watakayopangiwa, ikiwamo pembezoni.

Aidha, ada ya usajili na kumuona daktari kwa wanufaika wa NHIF kwa ngazi ya wilaya imeongezeka kutoka Sh. 2,000 hadi Sh. 7,000 kwa ngazi ya zahanati ada imeongezeka kutoka Sh. 1,000 mpaka Sh. 3,000.

Aidha, kitita hicho kitaboresha upatikanaji wa huduma bora za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wanachama.


Aidha, kitita hicho kimezingatia maendeleo ya teknolojia ya tiba, hali halisi ya bei katika soko na uwezo wa mfuko kugharamia huduma hizo huku ukiendelea kuwa endelevu kwa kuzingatia ushauri wa taifa, mapendekezo ya tathmini ya uhai na uendelevu.

Wizara ya Afya pia imetaja vipaumbele na kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa na kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya zahanati hadi taifa.

Katika bajeti hiyo wizara imetenga Sh. bilioni 117.61 kuimarisha huduma ya kinga dhidi ya magonjwa ikiwamo kuimarisha utekelezaji wa afua za chanjo kwa kuwafikia watoto 3,117,564 wenye umri chini ya miaka miwili, wasichana 871,429 wenye umri wa miaka tisa na wajawazito 3,298.437.

Kwa mujibu wa waziri, Sh. bilioni 17.18 zimetengwa kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, ikiwamo kujenga, ukarabati na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga wagonjwa waliozaliwa na uzito upungufu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tuungane kukemea mauaji ya wenzetu wenye ualbino

**KATIKA** kipindi cha miaka ya hivi karibuni, matukio ya mauaji ya watu wenye ulbino, ni kama yalikuwa yamekoma na kuwafanya wenye ulemavu huo kuishi kwa amani kwenye nchi yao.

Lakini ndani ya kimya hicho, matukio ya aina hiyo yameibuka upya, likiwamo lililochukua uhai wa mtoto mwenye ulemavu huo wa umri wa miaka miwili huko mkoani Kagera.

Tukio hilo la ukatili na la aibu kwa jamii, limewafanya watu wenye ualbino kuanza kuhofia uhai wao kama anavyoeleza Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania, Godson Mollel.

Waganga wa jadi wamekuwa wakihusishwa katika mauaji ya wenye uabino. Ninadhani ni vyema jamii ishirikiane na serikali kwa kutoa taarifa sahihi ambazo zitasaidia kuwakamata wahusika wa mauaji hayo na kuchukulia hatua za kisheria, ili kukomesha vitendo hivyo.

Ninaamini ushirikiano wa jamii ukiwapo, ni rahisi kutokomeza vitendo hivyo vya kinyama.

Hasa kwa kutoa taarifa kwenye vyombo vya usalama pale kunapokuwapo kiashiria chochote cha mauaji au kukatwa kiungo cha mtu mwenye ulemavu wa ngozi.

Inasikitisha kusikia kuwa waganga wa kienyeji huwaambia wateja wao kuwa viungo vya wenye ulemavu wa ngozi huleta bahati ya kupendwa, maisha marefu na mafanikio katika biashara.

Kuendekeza imani kama hizo kwenye baadhi ya jamii ni ukatili na aibu ambayo haipaswi kuvumiliwa na kila mpenda haki na anayeheshimu uhai wa mwenzake.

Hivyo jamii ingetoa ushirikiano na serikali kwa kuwafichua wale wote wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Ukatili huo unawanyima haki ya msingi ya kuishi na kuwaongezea ulemavu mwingine katika maisha yao bila hatia yoyote.

Hivyo, ushirikiano ukiwapo, Tanzania bila mauaji ya albino inawezekana.

Kama tunaweza kushirikiana katika mambo mengine, kwa nini tushindwe kushirikiana kwa ajili ya kutokomeza ukatili huo wanaofanyiwa binadamu wenzetu?

Vilevile, viongozi wa dini wasaidie kutoa elimu kwa waumini ili nao waipeleke kwa jamii kuhusu umuhimu wa uhai wa kila Mtanzania lakini wasaidie kuwafichua watuhumiwa.

Si sahihi kuamini kuwa mtu akiwa na viungo vya mwenye ualbino vitaweza kumsaidia kumletea mafanikio katika biashara, au atavua samaki wengi, kupata madini mengi machimboni au kupata cheo?

Watu wenye ulemavu wa ngozi au albino wamekosa nini hata wakatwe, viungo hata kuuawa? Kwa nini katika karne hii ya sayansi na teknolojia bado kuna watu wanaendekeza ushirikina.

Mauaji ya watu wenye ulemavu huo hayapaswi kunyamaziwa na jamii, kwani ni ukatili usio na mfano, walindwe dhidi ya matukio ya kutekwa ambayo mwisho wake huwa ni mauaji.

Ikumbukwe kuwa, watu wenye ualbino ni binadamu kama wengine wote, wana haki ya kuishi, wana haki ya kuwa huru katika nchi wanayoishi bila kutishiwa maisha yao kama ambavyo imekuwa ikitokea.

Pamoja na kuchukua hatua mbalimbali za kukomesha mauaji ya watu hao, ninadhani ipo haja ya kutolewa kwa elimu umma ili uachane na imani potofu inayosababisha kuwapo kwa mauaji hayo.

Kama kikwazo ni ukosefu wa elimu, basi umma uelimishwe, kama tamaa ya kutaka utajiri au kupata cheo, basi wahusika wachukuliwe hatua. Yaani yote hayo yafanyike ili wasiendelee kufanyiwa ukatili.

Ni vyema Watanzania kuheshimu uhai wa wenzao na kuacha kuua watu wenye ulemavu wa ngozi, badala yake wawalinde, kwani ni aibu kwa baadhi ya watu kuwaua au kushiriki kuwaua kwa lengo la ushirikina.

HABARI KITAIFA

# Wajasiriamali wapatiwa bilioni 995/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI 21,470 katika sekta mbalimbali wamepatiwa Sh. bilioni 995.346 na Benki ya CRDB kwa lengo la kuimarisha shughuli zao.

Hayo yamebainishwa wakati benki hiyo ikiadhimisha Siku ya Wajasiriamali Duniani, ikibainisha kuwa imetoa kiasi hicho cha fedha hadi kufikia Mei mwaka huu.

Vilevile, benki hiyo imeahidi kuendelea kuwezesha wajasiriamali mitaji nafuu na safari za kimataifa za kujifunza zaidi.

Ofisa Mkuu wa Uendeshaji wa CRDB, Bruce Mwile aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati benki hiyo ikiungana na wadau wengine kuadhimisha Siku ya Wajasiriamali Duniani kwa kuendesha semina kwa wateja wake na baadhi ya wabia wa kimkakati.

Sherehe za maadhimisho hayo zilifanyika makao makuu ya benki hiyo zikifunguliwa na ofisa huyo aliyesema kuwa kipaumbele chao siku zote ni kumhudumia Mtanzania na kuhakikisha anaboresha maisha yake kwa kumpa huduma zinazoendana na kukidhi mahitaji yake.

Ili kukuza ujasiriamali, Mwile alisema benki yao inatambua kuwa shughuli zake zikichangia asilimia 27 ya Pato la Taifa na ili itoe mchango wake ipasavyo kunahitajika huduma na mifumo shirikishi itakayosaidia wajasiriamali kuyafikia malengo waliyojiwekea.

"Kutokana na mikakati tuliyojiwekea, benki yetu imekuwa kinara katika uwezeshaji wajasiriamali kwani hadi Mei 2024, tulikuwa tumetoa zaidi ya Sh. bilioni 995.346 kwa zaidi ya wajasiriamali 21,470 katika sekta mbalimbali, zikiwamo za kilimo, ujenzi na makazi, miundombinu, usafirishaji, afya, elimu, nishati, madini, biashara na viwanda pamoja na uchumi wa buluu ili kuimarisha shughuli zao," alisema Mwile.

Alisema kuwa sekta ya ujasiriamali imekuwa kichocheo kikubwa cha ukuaji uchumi wa mataifa mengi duniani kwa kuchochea ubunifu na uanzishaji biashara mpya ambazo huongeza ajira na kuimarisha kipato cha watu binafsi na jamii kwa ujumla.

"Kwa kuanzisha biashara ndogo na za kati, wajasiriamali huchangia moja kwa moja katika ukuaji wa Pato la Taifa na kuongeza mapato ya serikali kupitia kodi. "Sekta hii pia ina mchango mkubwa katika kuboresha teknolojia na kuongeza ufanisi katika uzalishaji bidhaa na huduma, hivyo kufanya uchumi kuwa na ushindani zaidi kimataifa," alisema Mwile.

Taarifa za Umoja wa Mataifa (UN) zinaeleza kuwa wajasiriamali ni injini muhimu ya kufanikisha utekelezaji wa Maendeleo Endelevu (SDG) kwa kuwa kundi hilo linachangia asilimia 90 ya biashara zote duniani ambazo hutoa kati ya asilimia 60 mpaka 70 ya ajira zenye staha na kuchangia zaidi ya nusu ya pato la dunia.

Tanzania ina zaidi ya biashara ndogo za ujasiriamali milioni tatu zinazowapa uhakika wa kipato wamiliki wake.

Ili kumkuza mjasiriamali kuanzia ngazi ya chini kabisa, Mwile alisema Taasisi ya CRDB Bank Foundation ambayo ni kampuni tanzu ya benki yao, inatekeleza programu ya Imbeju inayotoa elimu ya ujasiriamali na fedha kwa wanawake na vijana pamoja na kuwapa mitaji wezeshi inayoanzia Sh. 100,000.

Hadi sasa, ofisa huyo alisema tayari programu hiyo imewafikia wajasiriamali zaidi ya 400,000 na kutoa mitaji wezeshi zaidi ya Sh. bilioni 10.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Royal Mark, Johnson Kapira, alisema kwa Mtanzania kuwa masikini kunatokana na kutokuwa na ujasiri wa kufanya uamuzi binafsi wa kuchangamkia fursa zilizopo.

Akieleza jinsi alivyoanza mwanzoni mwa miaka ya 1990 baada ya kuhitimu chuo kikuu, alisema kutokana na changamoto za kupata ajira zilizokuwapo, alianzisha kampuni yake na akawa anaomba mikopo ya kufanikisha kazi alizokuwa anazipata na mpaka sasa anakopesheka kiasi kikubwa zaidi.




Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainab Abdallah (katikati), akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wazee wa wilaya hiyo juzi kwa ajili ya kusikiliza changamoto na kero mbalimbali kwenye maeneo yao. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# 'Nchi za Afrika zitenge bajeti kudhibiti malaria'

**Na Joseph Mwendapole**

MWENYEKITI wa Umoja wa Viongozi wa Afrika katika Mapambano dhidi ya Malaria (ALMA), Sissoco Embaló amesema kuna haja nchi za Afrika kutenga bajeti ya kutosha kutoka vyanzo vya ndani ili kutokomeza ugonjwa huo.

Amesema uamuzi huo utakuwa na faida kubwa katika uwekezaji kwa kuwa wanatarajia kuona ongezeko la Dola za Marekani bilioni 127 kwa uchumi wa Afrika na kukuza biashara ya kimataifa kwa Dola za Marekani bilioni 81 ikiwa nchi zitafanikiwa kutokomeza malaria.

Embaló, ambaye ni Rais wa Guinea-Bissau, aliyasema hayo hivi karibuni alipozuru kikazi nchini na kutembelea ofisi za ALMA.

Alipongeza mchango mkubwa wa Tanzania katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria na kuomba ushirikiano zaidi ili kupata fedha za kutoka kwenye mfuko wa kimataifa.

Alisisitiza haja ya kustawisha uwajibikaji wa pamoja, mshikamano wa kimataifa na ushirikiano, ili kuhakikisha rasilimali zinazokusanywa zinalenga nchi na maeneo yenye maambukizi makubwa zaidi ili kuzisaidia nchi zenye uwezo mdogo wa kulipa.

Alitoa wito kwa nchi wanachama kuweka kipaumbele katika kuandaa ajenda na kutenga rasilimali katika bajeti za ndani ili kutokomeza malaria na alisisitiza umuhimu wa Bara la Afrika kuhakikisha wanakuwa na rasilimali muhimu ili kushinda mapambano dhidi ya malaria.

Mwenyekiti wa ALMA alibainisha kuwa maendeleo kuhusu udhibiti wa malaria barani Afrika yamedorora, akionya kuwa Bara la Afrika liko katikati ya dhoruba kali ambalo linatishia kuvuruga utoaji huduma muhimu za kuokoa maisha kutokana na ugonjwa wa malaria.

Alihimiza uhitaji wa haraka kwa nchi kuchukua hatua ili kupunguza athari mbaya zinazotokana na mgogoro wa kifedha duniani, kuongezeka kwa usugu wa viuatilifu na dawa za kutibu malaria, mabadiliko ya hali ya hewa na madhara ya kibinadamu.

Alisema tishio hilo linawakilisha dharura mbaya zaidi inayokabili malaria katika kipindi cha miaka 20 na itasababisha kuongezeka kwa malaria na milipuko iwapo haitashughulikiwa.

Alisema kuwa kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) tangu mwaka 2015, kasi ya maendeleo katika kupunguza visa vipya na vifo vitokanavyo na malaria imekwama katika nchi kadhaa.

Alisema kuwa Afrika iko nje ya mkondo kufikia malengo yake ya mwitikio na madhubuti yanayohusu malaria ya mfumo wa kichocheo wa Umoja wa Afrika katika kutokomeza UKIMWI, Kifua Kikuu na malaria.

Alisema kwa kutambua hitaji la dharura la kuiondoa Afrika kutoka katika dhoruba hiyo, Mawaziri wa Afya kutoka nchi za Afrika ambazo zina maambukizi makubwa ya malaria, wameahidi kuendeleza kwa kiasi kikubwa mapambano dhidi ya malaria na kuondoa vifo vinavyosababishwa na ugonjwa huo.

"Kupitia Tamko la Yaunde, nchi za Afrika zimejitoa kuongeza juhudi zao kupitia uongozi thabiti, uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya huduma za afya na mikakati bunifu ya kukabiliana moja kwa moja na ugonjwa huo," alisema.

Katika ziara yake, Rais huyo alishukuru Serikali ya Tanzania kwa niaba ya bara zima la Afrika kwa kuipatia ofisi Sektetarieti ya ALMA.


Pia alipongeza mchango mkubwa wa Tanzania katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria, ikiwa ni mojawapo ya vichochezi vya umaskini barani.

Ummy Mwalimu, Waziri wa Afya, alisema Tanzania imepiga hatua kubwa katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kulenga mpango sahihi wa afua ili kuongeza athari ya matokeo na hivyo kusababisha kupungua kwa vifo vipya vya malaria kutoka asilimia 50 mwaka 1990 hadi asilimia 8.1 mwaka 2022.

"Ni muhimu kwa Afrika kuweka kipaumbele katika utengenezaji bidhaa za afya, ili kuimarisha uthabiti na kupunguza utegemezi kutoka nje.

"Tanzania ndiyo mzalishaji mkubwa wa vyandarua vyenye viuatilifu, na inahitaji usaidizi wa ALMA ili kupitisha vyandarua vipya ambavyo vinafanya kazi vizuri kuzuia kutokea usugu wa viuatilifu," alisema.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Kanisa KKKT kuhudumia yatima afya, lishe

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KANISA la Kiinjili la Kirutheri Tanzania (KKKT) kupitia mradi wake wa Kizazi Hodari umekusudia kuwafikia watoto yatima na walezi wao 157,974 katika mikoa tisa nchini kwa kuwapa huduma mbalimbali ikiwamo kuboresha afya, ustawi wa jamii na lishe.

Mpango huo unaofadhiliwa kupitia Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) na kutekelezwa na KKKT umelenga kuwafikia watoto pamoja na wazazi wao watakaopatiwa huduma hizo kutoka mikoa ya Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Singida, Mwanza, Mara, Manyara na Geita.

Mkurugenzi Mshiriki Kanda ya Kaskazini Mashariki wa Mradi wa Kizazi Hodari kutoka KKKT, Issa Murshid, alisema hayo wakati akiwasilisha utekelezaji wa shughuli za mradi huo katika kipindi cha robo kwa wadau wanaoshirikiana na mradi huo.

Murshid alisema kabla ya kuwapa huduma watoto hao yatima kwanza wanaanza utambuzi na kuwasajili kupitia mifumo ya serikali pamoja na vituo vya afya ili kuwatengenezea mpango wa huduma gani wanayopaswa kupewa.

Alitaja baadhi ya huduma wanazotoa kuwa ni pamoja na mapambano dhidi Virusi vya Ukimwi (VVU), ikiwamo kupima watoto hao wanaobainika kuwa na maambukizi waanze kutumia dawa.

Hata hivyo Mkurugenzi Mshiriki Kanda ya Kaskazini Mashariki wa Mradi wa Kizazi Hodari, alisema mradi huo pia unaimarisha uchumi wa walezi wa watoto hao ili kuchochea utumiaji dawa.

"Ili kuhakikisha watoto walibainika kuwa na VVU wanatumia dawa za kufubaza tunahakikisha walezi wanawezeshwa kiuchumi kwani ukiwa na uchumi mbaya matumizi ya dawa yanakuwa ya mashaka," alisema Murshid.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dodoma, Josephine Mwaipopo, alisema kupitia mradi huo USAID Kizazi Hodari, wamewatambua watoto walio katika mazingira hatarishi na waliopata maambukizi ya VVU pamoja na waliokuwapo kwenye changamoto za kimaisha.

Alisema baada ya kuwatambua, watoto hao wameunganishwa na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwamo za kiafya, kupata elimu pamoja na kaya zao kuimarishwa kiuchumi.

Mkuu wa wilaya ya Idara ya Maendeleo ya Jamii Korogwe, Lutenganya, alisema mkoani Tanga, kupitia mradi huo wameibua watoto 1,559 wanaoishi kwenye mazingira hatarishi.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa akizungumza katika semina iliyoandaliwa na baraza hilo, kupitia programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA), kwa makundi ya kinamama, vijana na makundi maalumu, mkoani Mtwara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanufaika TASAF wapanda mikoko 200,000 kunusuru mazingira baharini

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

WANUFAIKA 29 kati ya 31 wa mpango wa kunusuru kaya masikini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), katika Kijiji cha Kondo Wilaya ya Bagamoyo, wamepanda mikoko zaidi ya 200,000 kwenye maeneo ya bahirini yaliyoathiriwa na shughuli za kibinadamu.

Mtaalamu msimamizi wa kikundi cha wanufaika wa mpango ambacho asilimia 75 ni wanawake, Juma Amani amesema mikoko hiyo imepandwa kwenye eneo la ekari 12.

Alisema katika eneo hilo mazingira yameharibiwa na kusababisha samaki kutoweka wakiwamo dagaa na kamba hali iliyookuwa inawapa wakati mgumu kwa watumishi wa rasilinali za baharini.

Kutokana na walichokifanya anasema maeneo mengine wameanza kuiga na kupanda mikoko kwenye maeneo kama hayo ambayo mazingira yake yanaharibiwa na shughuli za binadamu.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Pwani, Roseline Kimaro, amesema kabla ya mradi huo wananchi walikuwa wanakata miti na kusababisha samaki kutoweka na baada ya upandaji mikoko unaoendelea hali imeanza kubadilika na samaki wameanza kuonekana.

Mkurugenzi wa Uratibu kutoka TASAF, Haika Shayo amewapongeza wanufaika hao kwa kutekeleza shughuli za mpango huo kwa kupanda mikoko ambayo inakwenda kuzuia mmomonyoko na kupoteza rasilimali za baharini.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Jafary Athuman, alisema wananchi walichukua hatua hiyo baada ya kuona athari za uharibufu wa mazingira ambao umeanza kukikumba kijiji hicho ikiwamo mazalia ya samaki kutoweka na kuongezeka kwa kina cha maji.

Mmoja wa wanufaika, Mwanaheri Maulid, ameshukuru TASAF ilivyomsaidia kujikwamua na hali ya umasikini kutokana na ruzuku wanayopatiwa kusaidia kusomesha watoto na kuanzisha miradi ya kuwaingizia kipato.

Wataalamu kutoka Mfuko huo wakiambatana na wadau wa maendeleo wamefanya ziara kwa wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya masikini kufuatilia utekelezaji wa mpango kwa wanaoendelea na mpango na ambao tayari wametoka baada ya hali zao kuimarika katika Wilaya ya Bagamoyo.

# Ruvuma waazimia usimamizi kudhibiti moto vijiji vyote

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WADAU wa maliasili mkoani Ruvuma wameazimia kuweka vijiji vyote kwenye mpango wa usimamizi jumuishi ili kukabiliana na tatizo la moto.

Maazimio hayo yamepitishwa kwenye kikao cha wadau hao kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Peres Magiri.

Kikao hicho kimefadhiliwa na mradi wa panda miti kibiashara na kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wawakilishi kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), mameneja wa mashamba ya miti ya serikali, Mwakilishi kutoka Chuo Kikuu cha SUA na wawezeshaji wa majanga ya moto na usimamizi wa moto vijijini.

Mwezeshaji Andrew Fernand akizungumzia usimamizi wa moto vijijini, alisema mpango huo unatekelezwa katika halmashauri 10 nchini katika kipindi cha miaka mitano na ameitaja moja ya halmashauri hizo ni Madaba iliyopo mkoani Ruvuma.

Alisema programu hiyo katika Halmashauri ya Madaba inatekelezwa katika kijiji cha Wino na kwamba ili kutekeleza mpango huo kila halmashauri itakuwa na msimamizi wa masuala ya moto.

Alisema mpango wa kupambana na moto katika Halmashauri ya Madaba unatekelezwa katika vijiji saba na vyote vimeweka sheria zinazosaidia kukabiliana na majanga ya moto unatokea hasa katika kipindi cha kiangazi.

Kadhalika, kati ya vijiji saba vinavyotekeleza mpango huo ni kijiji kimoja pekee cha Wino chenye mfuko wa fedha wa kupambana na moto na kwamba vijiji vinne kati ya saba vimenunua vifaa vya kupambana na majanga ya moto.

"Chanzo kikuu cha moto ni wakulima wanapoandaa mashamba yao, wananchi wanatakiwa kubadilika kifkra kuhusu kuandaa mashamba kwa kuchoma moto, elimu inatakiwa kuwa endelevu pamoja na ununuzi wa vifaa vya kukabiliana na moto," alisema.

Mwakilishi wa Meneja Hifadhi ya Misitu Wino Madaba, Goffrey Shio, amesema shamba hilo limepanda zaidi ya miti hekta 5,000 ya aina mbalimbali na kwamba hifadhi hiyo katika kipindi cha mwaka 2012 hadi 2024 imeotesha jumla ya miche milioni 8.8.

Hata hivyo, amesema wakulima wenye mashamba ya mabondeni huandaa mashamba yao kwa kutumia moto na kila mwaka unaleta madhara makubwa kwa kuunguza mashamba ya miti ya wananchi na mwaka 2023 zaidi ya hekta 3,000 za mashamba ya miti ya wananchi ziliteketea.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Ruvuma, SF Melenia Nyabwinyo, aliomba kuimarisha ushirikiano baina ya Idara ya Zimamoto na wadau wa misitu pamoja na wananchi kwa kutoa taarifa mapema za matukio ya moto ili kufanya uchunguzi wa moto kwa wakati.

Nyabwinyo alitoa rai kwa TFS na wamiliki wa misitu kuwalipa posho zao kwa wakati wafanyakazi wanaojitolea kulinda mashamba ya miti na misitu yao ili wasiweze kuhujumu kwa kuanzisha moto baada ya kuchelewa kuwalipa maslahi yao.

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Magiri alisisitiza elimu ya kukabiliana na mto iwe endelevu na itolewe kuanzia ngazi ya vijiji.

Alisisitiza kila kijiji kianzishe kamati na vikosi vya kukabiliana na matukio ya moto pamoja na kutoa mafunzo ya mara kwa mara na ununuzi wa vifaa vya kuzimia moto ili kulinda rasimali za misitu.

"Majukumu ya kuanzisha kamati za moto za vijiji tumekubaliana kuanzia Julai mwaka huu na kutoa elimu na namna ya kuunda mfuko wa fedha kwa ajili ya vijiji kuhusu suala la moto," alisisitiza Magiri.

Ametaka wadau kuanzia ngazi kamati za vijiji hadi wilaya washirikishwe kwenye mpango jumuishi wa vijiji kukabiliana, kudhibiti na kuzuia majanga ya moto.

Pia, wadau wa misitu wana kazi kubwa ya kuwaelimisha wananchi vijijini na wadau wote ili wapate taarifa sahihi katika kudhibiti matukio ya moto.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# RE- ADVERTISEMENT

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

## 1. POSITION: CAPTAIN - (30 POSTS)

### 1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:

- Must have flown with more than 3500 flying hours with an Airline Transport Pilot License, Multi Engine and Instrument Rating.
- Must have 1000 hours as a Pilot in Command and an experience of handling a minimum of 20 tons equipment or above with a good performance.

### 1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- Responsible for safety of the aircraft, its occupants and cargo pre, during and post flight.
- Maintain a high standard of discipline, appearance, uniformity and promptness of Co-pilots and Cabin Crew.
- Determine the achievement of commercial aspects of flights safety is not impaired to obtain additional revenue load for the Company.
- Ascertain that Flight Plans, Notam, Fleet Notices, Weather and any pertinent documentation and service items that flight may require are briefed.
- Verify that the loading of aircraft being performed in accordance with laid down procedures.
- Report all incidents and accidents.
- Verify that all documents/certificates required being on board the aircraft are available and valid.
- Report any Flight delays of flights.
- Accept and sign for diplomatic mail, precious cargo and supervise stowage aboard the aircraft and handover to destinations.
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

## 2. POSITION: FIRST OFFICER - (13 POSTS)

### 2.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:

- Must have flown with more than 250 flying hours or above with Commercial Pilot License, Multi Engine with Instrument Rating.
- Must be with an experience of handling a minimum of 10 tons' equipment with good performance.

### 2.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- To participate in the Pilot-in-Command's crew briefing, and make himself aware of all relevant aeronautical and meteorological information as well as relevant papers documenting the aircraft technical status and its anticipated load.
- To prepare the OFP and when necessary, file the ATS Flight Plan with the appropriate Authority. If stored plans are used then he should ensure that the correct plan has been activated
- To carry out such duties concerning the flight in accordance with the SOP, including procedures, limitations and performance related to the specific aircraft type, as allocated to him by the Pilot-in-Command;
- To confirm the safe navigation of the aircraft, maintaining a continuous and independent check upon both the geographical position of the aircraft and its safe terrain clearance
- To safely and properly conduct the flight in compliance with the current flight plan and the Pilot-in-Command's instructions when the Pilot-in-Command is not at the controls. Any change to the current flight plan has to be notified to the Pilot-in Command.
- To provide advice, information and assistance to the Pilot-in-Command, as may contribute favorable towards the safe and efficient conduct of the flight.
- To assist the Pilot-in-Command in administration duties related to the flight and
- To seek and receive information and/or explanation from the Pilot-in Command, as may be necessary to enable fulfilment of functions.
- To assist the Flight Safety Department for all Technical related matters
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

## 3. TERMS AND CONDITIONS:

Ten (10) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

## 4. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council- NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

## 5. CLOSING DATES:

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Issued on 28th June, 2024**

ATCL is an equal opportunity employer. Women are encouraged to apply. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.





# Polisi watoa tahadhari kukithiri noti bandia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga limewataka wakulima wanaouza mazao katika msimu huu kuepuka kupokea fedha nyakati za usiku, kutokana na kukithiri kwa fedha bandia za Sh. 10,000.

Rai hiyo imetolewa na Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kennedy Mgani, baada ya kukamata noti bandia za Sh. 10,000 zenye thamani ya Sh. 420, 000 pamoja na vitu mbalimbali vilivyokamatwa kwenye operesheni inayoendelea mkoani hapa.

"Fedha hizi za noti bandia za Sh.10,000 tumezikamata katika matukio mbalimbali zikitumika katika manunuzi, hivyo tunapenda kuwatahadharisha wakulima wanapouza mazao yao wawe makini wakati wakipewa malipo," alisema Kamanda Mgani. Aidha, alisema katika msako huo walikamata pia vielelezo mbalimbali vya wizi, ikiwemo silaha moja ambayo ilitumika katika tukio la unyang'anyi katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

Pia, walikamata mabomba 10 ya maji, pamoja pikipiki tano, vifaa vya kupiga ramli chonganishi, mtambo mmoja wa kutengenezea pombe, televisheni moja, meza mbili, kabati la kuwekea televisheni, milango miwili pamoja na madirisha manne ya chuma.

Alisema katika msako huo wanawashikilia watuhumiwa 25, kwamba upelelezi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Aidha, kwa upande wa usalama barabarani mkoani humo, alisema makosa 3,438 ya magari yalikamatwa na makosa ya pikipiki na bajaji yalikuwa 1,496, huku dereva mmoja akifungiwa leseni yake kwa kukiuka sheria.

Kadhalika, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kushirikiana na Jeshi hilo kwa kutoa taarifa za uhalifu, pamoja na madereva kuzingatia sheria za usalama barabarani.



Wanafunzi wa Chuo cha Biblia cha Tanzania Assemblies of God (TAG) Kanda ya Ziwa, wakichangia damu salama jijini Mwanza jana, kwa ajili ya kuokoa maisha ya watu wenye uhitaji, kuelekea maadhimisho ya miaka 85 tangu kuanzishwa kwa kanisa hilo, yanayotarajia kufanyika leo. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Waombwa kuchangia damu kunusuru maisha ya wagonjwa

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

JAMII imeombwa kuchangamkia fursa ya uchangiaji damu salama ili kunusuru maisha ya watu wenye uhitaji hususani wajawazito, watoto na waliopata ajali.

Ombi hilo limetolewa na Mkuu wa Chuo cha Biblia cha Kanda ya Ziwa cha TAG, Mchungaji Exaud Lisulile, wakati wa utoaji damu katika kanisa hilo.

Alisema wamepata nafasi ya kuigusa jamii kwa utoaji damu kwamba inakwenda kuokoa maisha ya watu.

Alisema utoaji wa damu ni moja ya kazi ambayo Mungu amewataka waifanye, hivyo aliwaomba wananchi kutokuwa na hofu yoyote juu ya utoaji damu.

"Uchangiaji damu siyo dhambi bali ni utekelezaji wa kile Mungu anataka kifanyike, katika kuokoa maisha ya watu ukiona mtu anaumwa alafu ukapita kando na kwenda zako utakuwa hujatimiza kile Mungu anataka. Shughuli hili ni kutekeleza adhima ya kile tunachotakiwa kukifanya" alisama Lisulile.

Naye, Jeremiah Sabato Mratibu wa shughuli za utoaji damu alisema suala hilo ni moja ya hatua ya kuelekea maadhimisho ya miaka 85 tangu kuanzishwa kwa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) nchini, wamefanikiwa kupata watu takribani 50 waliojitolea kuchangia damu japokuwa lengo lilikuwa ni kupata watu 100.

"Maadhimisho hayo yanayotarajia kufanyika leo Juni 28 mwaka huu, tumefanya mambo mbalimbali ikiwemo kutoa huduma kwa jamii mfano kutengeneza barabara, kutembelea hospitali na kufanya usafi kwenye maeneo mbalimbali,"alisema Sabato.

Aidha, Mratibu wa Damu Salama Halmashauri ya Ilemela, Martine Machela alisema kuwa mahitaji ya damu ni makubwa, inachangiwa na watu kutokuwa na mwitikio wa kuchangia.

Alisema mahitaji yao ni makubwa hasa kwa wajawazito, watoto chini ya miaka mitano wenye selimundu, hivyo aliwaomba wananchi kujitokeza na kuondoa dhana ya kuwa ukitoa damu unakuwa dhaifu.

Mmoja wa wachangiaji damu, Stella Thomas alisema kuwa ameguswa na utoaji damu ili kuokoa maisha ya ndugu, marafiki.

# Tanzania yajumuishwa utafiti hali ya hewa na mazingira

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TANZANIA ni miongoni mwa nchi iliyojumuishwa katika utafiti wa uandishi wa habari za hali ya hewa na mazingira duniani, ambapo habari hizo zimeongezeka kwa kiasi kikubwa kulinganisha na ilivyokuwa hapo awali.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Internews Earth Jounalism, James Fahn ilieleza kuwa ripoti ya hivi karibuni ya Internews iliyofanywa kupitia mpango wake wa uandishi wa habari za mazingira, limetoa tathmini ya kina kuhusu hali ya uandishi wa habari za hali ya hewa na mazingira duniani. Alisema katika tathmini hiyo, matokeo hayo kwa Tanzania yameonyesha kuwa kuripoti habari hizo zinaonekana kuongezeka.

Ripoti hiyo inaonesha kwamba asilimia 82 ya waandishi wa habari duniani kote walikubali kuwa habari za hali ya hewa na mazingira kwa sasa zina umuhimu zaidi, ikilinganishwa na miaka kumi iliyopita.

"Licha ya ongezeko hili, ripoti hii inaonesha kwamba waandishi wa habari wanakubali habari za mazingira wanazoripoti hazitoshi ukilinganisha na mbadiliko ya tabia nchi na hali ya hewa" ilieleza ripoti na kuongeza:

"Ripoti inaonyesha kwamba waandishi wengi wanaandika habari za hali ya hewa na mazingira kwa kuangalia zaidi katika mtazamo wa afya kwa asilimia 70, wakisisitiza uhusiano kati ya uharibifu wa mazingira na afya ya jamii".

Aidha, mada nyingine zilizopewa kipaumbele mara nyingi ni pamoja na ukataji wa miti kwa asilimia 62, maji na usafi wa mazingira asilimia 58, sera za serikali kwa asilimia 56, na uchafuzi wa plastiki kwa asilimia 53 na hakuna aliyewajibishwa kisheria.

Ripoti hiyo pia ilieleza kuwa pamoja na mafanikio adha kadhaa zinazowakabili waandishi wa habari wanaoandika habari za masuala ya hali ya hewa na mazingira ni ukosefu wa fedha, taaluma na kukosa ushirikiano wa vyombo wanavyofanyia kazi, kwa kukosa msukumo au kipaumbele wanapowasilisha kazi hizo.

# MSD yaboresha huduma za ugavi kwa asilimia 80

**Na Remy Moka,** SAUT

MKURUGENZI Mkuu wa Bohari ya Dawa ya Taifa (MSD), Mavere Tukai, amesema bohari hiyo imefanya maboresho katika utoaji huduma za ugavi zinazokidhi mahitaji ya mteja, kutoka asilimia 41 mwaka 2021/22 hadi asilimia 80 kwa mwaka 2023/24.

Aliyasema hayo juzi jijini Mwanza wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa wateja na wadau wa MSD Kanda ya Mwanza, uliolenga kujadiliana juu ya utatuzi wa adha za upatikanaji wa bidhaa za afya.

Alisema licha ya maboresho hayo makubwa bado wanahitaji kufanya juhudi zaidi ili kuhakikisha wanafikia uhitaji wa kila mteja na kukidhi mahitaji yake.

"Uwezo wa MSD kutunza dawa kitaifa umeongezeka kwa asilimia 12, ndiyo maana tunaona kwa sasa malalamiko yamepungua na lengo la kisera kwetu ni kuwa na mzigo hata wa miezi mitano, kwa wakati wowote ili ikitokea mzigo umechukuliwa hatuwezi kufikia akiba ya sifuri," alisema Tukai.

Aidha, alisema kwa sasa wamepunguza madeni ya wateja ambapo imefikia hatua ya pamoja ya kudai na kudaiwa, licha ya kuendelea kuboresha usambazaji wa dawa.

Alisema pia imeingeza uwezo wa kusambaza vifaa tiba ambapo umeimalika kwa zaidi ya mara mbili pamoja na huduma za meno.

"Hii inatokana na misingi tuliyoiweka katika maeneo ya manunuzi, uboreshaji wa mfumo wetu wa ndani wa usimamizi pamoja na uhusiano mzuri na wateja," alisema Tukai.

Kuhusu Kanda ya Mwanza, Tuka alisema bohari hiyo imezidi kuimarisha upatikaji wa dawa katika vituo 1,337 vya kanda hiyo ambapo Hospitali ya Rufani ya kanda moja, mikoa mitano, zahanati 1,137 na nyingine binafsi 18 ," alisema Tukai.


Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Yudas Ndungile, aliishauri bohari hiyo kuendelea kuboresha huduma zake kwa kuwa na vifaa vya kutosha, vifaa tiba vya huduma za kibingwa ili kuendana na maboresho makubwa ya miundombinu katika sekta ya afya.

Alisema: "Ni jukumu lao kujua aina ya miundombinu ambayo inaendelea kuboreshwa katika hospitali, vituo vya afya pamoja na zahanati, ili wao wawe mbele yetu kwa kununua vifaa mapema kabla ya sisi hatujamaliza majengo ili tukimaliza ujenzi tufanye manunuzi ya vifaa tiba vinavyoendana na majengo hayo," alisema Dk. Ndungile.

Ukurasa 12



TANGANYIKA NA SAFARI YA UHURU...
Jozi za harakati siasa zilivyoundwa katika mzizi mmoja na nyendo maendeleo nchini




**Safari ya Korea na mauzauza yake -II**

Ukurasa 13


# BUFE
IJUMAA JUNI 28, 2024
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


## IMARISHA UCHUMI NA MAMA SAMIA

# Programu ya Rais inayomea kwa kasi kuwanasua waliko kimkoa

## •Ma-RC Dar, Moro wazindua na ahadi tele

**Na Mwandishi Wetu**

KUANZIA mwezi uliopita nchini, kulitawaliwa na mshikemshike wa kuasisiwa kitaifa Programu ya Kitaifa iliyobuniwa na Rais Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Ni programu iitwayo; Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA), ambayo, mtazamo mkuu hapo, unalenga kumwezesha na kumwibua mwanamke kutoka shimo la lindi la umaskini, kupitia mikopo kwenye vikundi makundi maalum ili kuwafikia walengwa.

"Juhudi za kila siku za shughuli za kijasiriamali ndio zitakazotutoa kimaisha na kuendelea kuchangamkia fursa za kiuchumi," anasititiza Adam Malima, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, mwezi Mei.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng"I Issa, akizungumza na viongozi wa Mkoa wa Morogoro katika uzinduzi wa programu Imarisha Uchumi na Mama Samia.Kushoto kwake ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Dk. Mussa Aly Mussa. **PICHA: MTANDAO.**

Programu hiyo imeandaliwa na Rais, kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), ambako katika mwezi huo, mkoani Dar es Salaam walikuwa sehemu ya harakati hizo, kutumia fursa za kibiashara zinazopatikana kuanzisha shughuli za ujasiriamali na biashara.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alipozindua Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA) mkoani kwake, akisema kuna umuhimu wa kinamama kuzichukua changamoto na matatizo, kuwa fursa za kuinuka kiuchumi.

Anasema hayo katika uzinduzi wa programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia (IMASA), mwezi uliopita inayotekelezwa na baraza hilo, ndani ya Dar es Salaam.

Mkuu wa Mkoa Chalamila na ufafanuzi: "Kwa sasa mkoa huu unajipanga kuendelea kujenga masoko makubwa ya kisasa katika kila wilaya na kama mnavyojua kwamba Soko la Kariakoo, linajengwa kisasa zaidi na lipo katika hatua za mwisho."

Hapo anaeleza kwamba, Rais Dk. Samia hivi sasa ana ndoto za kuwawezesha wanawake nchini kiuchumi, kwa kutaka kuwaunganisha na biashara, pia fursa zitokanazo na miradi ya kimkakati unayoendelea nchini.

**BARAZA LA UWEZESHAJI**

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Beng` Issa, anasema baraza lake kupitia Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia, iko katika hatua za kuwakwamua wanawake, vijana na makundi maalumu kufanya shughuli zao za kijasiriamali.

"Baraza linatambua mkoa wa Dar es Salaam, unahitaji maeneo kwa ajili ya kusindika mazao yao, kuwa na masoko (super market) ili wateja waweze kwenda kununua bidhaa zilizotengenezwa hapa nchini," anasema.

Anaeleza kuwa, baraza hilo limejipanga kuwaunganisha wanawake na taasisi mbalimbali ikiwamo ya Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) pamoja na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), kupata mustakabali wa teknolojia na vibali mbalimbali.

Anawataka wanawake mkoani Dar es Salaam, kuwa na nidhamu ya fedha, ikiwamo kuweka fedha katika akaunti na sio vibubu, ili kuendeleza biashara zao.

"Jiungeni katika vikundi vya VICOBA ili kusaidia kuweka fedha na kukopa kwa vile mnakopeshana kwa riba nafuu na kujiepusha na ukopaji katika vikundi vya kausha damu," anasema.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, hadi sasa serikali ina mifuko mingi ya uwezeshaji mikopo, katika mfumo unaofuata masharti.

Anaitaja programu hiyo inayonadiwa, ina jukumu kubwa la kuwaunganisha wanawake nchini kutumia fursa zilizopo, akisema baraza lao husika limeanza kupeleka programu ya ufundishaji wa ujasiriamali shuleni, kuanzia shule ya msingi, sekondari hadi vyuoni.

"Kwa sasa kitakwimu kuna wajasiriamali milioni tano na asilimia 54 ni wanawake nchini nzima. Baada ya uzinduzi wa programu, ni matarajio yetu wanawake wataendelea kujitokeza kwa wingi," anasema.

Anafafanua kwamba kupitia baraza hilo, wameanza kuwafundisha na kuwasaidia kinamama kuandika na kuomba zabuni kwenye halmashauri katika juhudi za kuwajengea uwezo wanawake.

Anataja programu hiyo inalenga kuboresha uchumi wa mwanamke, kijana, mzee, mlemavu na makundi maalum, ili kuweza kuwainua kutoka lindi la umasikini.

"Tumeambiwa na wanawake kwamba, wajasiriamali wanataka kutegemewa maeneo ya kufanya

Inaendelea Uk 14

UCHUMI

TANGANYIKA NA SAFARI YA UHURU...

# Jozi za harakati siasa zilivyoundwa katika mzizi mmoja na nyendo maendeleo nchini

- Jumuiya Wafanyakazi iliyomuibua Kawawa
- Mama wauza pombe, wadau Yanga Jangwani



Wanaharakati wa Uhuru wa Tanganyika, waliokusanyika katika makao makuu ya chama cha TANU, Magomemi Mapipa, Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

**Na Peter Orwa**

KIHISTORIA, ni ngumu kutenganisha siasa na uchumi. Pia, ubia huo mara zote huzaa mabadiliko ya hatua mbele kwa idadi na tija ya vitu na huduma, ikizaa kinachoitwa maendeleo.

Wakati siasa ni mbinu, mikakati na namna ya kushika nafasi na mamlaka ya kumiliki, pia kusimamia uendeshaji wa rasilimali za umma na maslahi yake; inaporejewa jinsi gani rasilimali hizo zinatumiwa kwa stadi bora, kunufaisha maslahi mapana ya umma, hapo kunapatikana maana ya uchumi.

Hiyo ndio tasfiri ya msemo 'siasa ni uchumi na bidhaa yao ni maendeleo,' na vyote hutegemea na sura tofauti. Hapo ndiko kunakopatikana historia ya siasa nchini, inavyofungamana na mipango yake ya uchumi na maendeleo.

Awali, Watanganyika wakiwa katika harakati zao kusaka maendeleo, wakianza na chama chao cha kijamii TAA kukua kwa nyendo zake, nyuma ya pazia kukawapo rafiki yao Jomo Kenyatta, Mwenyekiti wa chama kama hicho, lakini zaidi cha kisiasa, KAU nchini Kenya, kukizaa matunda.

Kutembeleana baina ya Kenyatta na viongozi wa TAA, chama kilichoasisiwa mwaka 1922, akiwamo muasisi Abdulwahed Sykes, kulizaa matunda ya utashi wa kisiasa na mikakati, hatimaye mwaka 1952 wakawa na mwanachama wa karibu, kijana mwerevu na mwalimu wa Shule ya Sekondari Pugu, Dar es Salaam, Julius Nyerere.

Ni mageuzi yaliyobadili utashi, kwani baada ya mwaka mmoja, Oktoba 10, 1953 Mwalimu Nyerere, aliyepewa uenyekiti, akabuni mikutano ya kimkakati ya TAA, kila Jumamosi, akijumuika na wenzake; Abdulwahid Sykes, Ally Sykes, Dossa Aziz na John Rupia, kujadili namna ya kuibadili TAA kuwa chama kamili cha siasa.

Hatimaye Julai 5 mwaka 1954: TANU ilianzishwa na wajumbe wa mkutano walibadili katiba ya TAA kuwa TANU, Hao walikuwa: Abdulwahid Sykes, Julius Nyerere, Tewa Said Tewa, Dossa Aziz, Ally Sykes, Kasela Bantu, Abubakar Ilanga na Saadan Abdu Kandoro.

Wengine walikuwa Suleiman Kitwala, Oswald Milinga, Patrick Kunambi, Gerimano Pacha, Japhet Kirilo, Makaranga, Joseph Kimalando na John Rupia.

### NYERERE ALIVYOIBUKA MTAANI

Kuiasisi TANU kuliendana na hatua za Nyerere, kuvianisha vikundi vya kijamii mtaani, alivyoamini iwapo vingemuunga mkono, basi mafanikio ya uhuru anaodai yangekuwapo.

Hapo kunatajwa vikundi vya vijana, wazee, kinamama, wakulima na wafanyakazi. Ndio ukawa mwanzo wa nyendo za uhuru nchini, hadi mafanikio yake kukiwapo majina kama ya Waziri Mkuu, Rashid Kawawa na Waziri Bibi Titi Mohamed.

Pia, hata katika mustakabali wa burudani ya soka nchini, timu ya soka ya Yanga leo ikiitwa jina la masihara 'Klabu ya Wananchi' chimbuko lake ni kwamba ilitumika sana katika siasa za vijana wakati huo, kufanikisha nyendo za TANU.

Wakati fulani, Waziri Mkuu Mstaafu Rashid Kawawa, katika mazungumzo naye na mwandishi wa makala hii, akafafanua namna 'alivyomkosha' Mwalimu Nyerere kufanikisha mgomo wa Shirika la Reli ulikuwa na tija kwa siasa za TANU, ambayo ilikuwa harakati za kimaendeleo kwa Watanganyika.

Nyerere alivutiwa nayo na kuiingiza katika mtaji wa harakati za siasa za uhuru kwa Tanganyika inayosaka uhuru, huku Mama Bibi Titi Mohamed akitokana na kundio la kinamama wapika pombe, Karikakoo.

Ndicho kikarejewa katika mazungumzo na Mama Maria Nyerere, Butiama kuhusu 'TANU na Yanga' kabla ya uhuru na kazi ya Joseph Nyerere mdogo wa Mwalimu Nyerere, alivyokuwa mdau wake.

Ndani ya siasa hizo kusaka uhuru, Mwalimu Nyerere, alishajijengea mwenendo wa siasa Tanganyika ingefuata kujijengea uchumi na maendeleo ya watu wake.

Wakati huo, aliandaa safu hiyo ya siasa, hata akafanikiwa kumhamisha Katibu Mkuu Kawawa, kutoka chama cha wakafanyazi wakati huo, TFL, hadi akawa mtendaji wa nafasi inayofanana na hiyo ndani ya TANU, sambamba na orodha ya wengineo.

Pia, siasa za dunia zikiwa zimepamba moto wakati huo, Nyerere akajiwekea msingi wa siasa zake za maendeleo, iwapo uhuru ungepatikana. Hizo zilikuwa siasa za kijamaa.

Kimsingi, ni kipindi ambacho dunia ilikuwa imegawanyika katika ngome kuu mbili, Mashariki ikiwa na nchi zenye mlengo wa kijamii zikiongozwa na iliyokwa Muungano wa Urusi au USSR, pia zikawepo nchi za Ulaya Mashariki, waumini wa ujamaa.

Vilevile, kuwapo ngome ya magharibi zikiwamo nchi Marekani na Ulaya Magharibi, zilizotawala makoloni mengi, wakiwa waumini wa siasa na uchumi huria, Sababu ya Nyerere na TANU kuzama katika matazamo wa kijamii, ililenga vigezo kadhaa. Mosi, ni kwamba, koloni la Uingereza ilishajiwekea kutodumisha utawala huo wa ukonini, ikiwkea taifa kipindi cha mpito.

Hiyo ilikuwa tofauti, kama ilivyo kwa Kenya na Southern Rhodesia (Zimbabwe), ambako kumekuwapo uwekezaji mkubwa kuanzia na majengo, miundombinu, mashamba makubwa mahitaji ya lazima kama elimu na tiba.

Pia, katika elimu ni Watanzania wachache sana walipata fursa ya kwenda shule, nafasi kubwa wakipewa Wazungu, kufuatiwa na Waasia, hata kufanya kundi kubwa la wazawa wakiwa katika hali ya chini kitaaluma.

Kisiasa, pia nchi za Mashariki na hasa USSR zilishaonyesha urafiki wa kuunga mkono mataifa ya Kiafrika yaliyokiwa yanajikomboa na ukoloni, hata kutoa fursa za kujisogeza kwa elimu ya juu.

### TANGANYIKA ILIVYOONA UHURU

Mnamo Disemba 9, 1961 kupatikana uhuru wa nchi, uongozi kukabidhiwa kwa Rais Nyerere, ukawa mwanzo wa taifa jipya Tanganyika.

Nyerere alipokea nchi, ikiwa na kasoro nyingi za kimaendeleo, kama walioelimika wachache hata nchi kukosa watalamau kuiendesha, huduma za mahitaji muhimu kama elimu na afya, hali kadhalika viwanda vichache vilivyokuwapo vililenga mahitaji kama vile; kuandaa malighafi ya kusafirishwa nje na mavazi nchini.

Hapo ndipo Mwalimu Nyerere akasimama na hoja kwamba "Hadi sasa tunazalisha tusivyotumia na kutumia tusivyozalisha" kukishuhudiwa malighafi mengi ya shamba yanapelekwa nje ya nchi na uagizaji mahitaji mengi yanatoka nje ya nchi.


Baada ya uhuru, Rais Nyerere akaanza kwanza, kuhamia katika chama cha TANU akikiboresha ana kumuachia Kawawa uongozi wa nchi, baadaye akarejea nafasi yake na kukaundwa Jamhuri ya Tanganyika, mwaka 1962.

Ilikuwa hatua iliyoendana na kufungua milango shule kuwa ya watu wote, ili kuapta Watazania wengi wasomi, kuboresha kilimo na soko lake; vote vikiingia katika Mpango wa Mandeleo wa Miaka Mitatu ya Tanganyika hadi kufikia 1964.

Ndani ya kipindi hicho miaka mitatu, Rais Nyerere alifungua urafiki na baadhi ya nchi za ughaibuni na hasa Mashariki, hali kadhalika mtawala wake kikoloni, Uingereza. Wapo waliopata fursa kwenda kusoma ughaibuni, kisha wakarudi kama wataalamu wa nchi.

Kufika mwaka 1964, ishara ya taifa kung'ara na sura ya mapinduzi ilionekana, taifa likodinga katika maendeleo na mageuzi ya kisiasa, zikishikamana katika sura ya jozi.


***• Ijumaa Wiki ijayo usikose simulizi ya mageuzi makuu uchumi baada ya miaka mitatu, inavyodumu kuwa kigezo kikuu cha mipango na dira ya nchi hadi sasa.***



Rais Julius Nyerere, na Waziri Mkuu wake, Rashid Kawawa. Katikati ni mgeni wao Rais wa Zambia, Kenneth Kaunda.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Safari ya Korea na mauzauza yake -II






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

WIKI jana tuliishia pale tulipokwenda migahawani kutafuta chochote kitu cha kutia tumboni, baada ya pale hotelini kuambiwa 'jipaka limelala jikoni', hivyo ikabidi kujitafutia wenyewe kama mipaka ya baa.

Kuingia tu pale mgahawani, tukaletewa orodha ya vyakula vilivyopo, mnaita menyu, hapo tukajikuta tukifurahia nyoyoni kuwa tutakula mikuku tunavyotaka.

Kama nilivyosema wiki jana, vyakula ni kuku na mbatata, yaani chipsi kurahisisha ila ukipenda ita Chimaek.

Tulikuwa watatu, hivyo tukasema kila mtu aagize sahani yake tuone kama tutatosheka, hasa tukiona vijamaa vyao vidonyo vidonyo, hivyo tukaamini hata vijisahani vitakuwa hivyo.

Wale wahudumu wetu, walipotuzoea na kujua tunatoka Tanzania, kila mara walituita 'Tanjania', hakika wakitufurahia sana kama ambavyo nasi huwa wakarimu tukutanapo na wageni, hususan watokao nje na si wa mtaani kwetu.

Baada ya muda huku wakitushangaa kutokana na miili tulivyojazia jazia hususan maeneo ya tumboni na hata huyu bibie tuliyefuatana naye, dakika 20 hivi sahani zikaletwa! Eh bwana weee! Tulichokiona si tulivyodhania.

Mikuku hiyo, ya kuchoma na kukaanga, kila mmoja kuku wake na si vijikuku ni mikuku, mikubwa. Tulipouliza kwa nini mikubwa vile, wakatujibu kwao hawanaga masuala ya nusu, sijui robo kuku.

Ukiagiza kuku, anakuja kuku aliyeondolewa manyoya, utumbo, kichwa na miguu tu! Vingine vyote shauri yako na tumbo lako.

Tulitazamana na kucheka. Tukaomba tena kitabu cha menyu tujikumbushie bei, isije ikawa tunanunua kwa posho yote ya siku moja!

Kitabu kilionyesha bei ile ile ya won 18,600 kwa sahani, yaani ukiwa Bongo ni Sh. 37,200 kwa sahani ya chipsi kuku.

Unafanyaje sasa, kwa sababu hakuna kukata nusu au robo, ni kufakamia mpaka mwisho ndipo utaamua kama ni kusaza, kumwaga au kufunga.

Busara ikatujia kuwa tuanze na sahani mbili na kama tutashindwa kuendelea kushambulia ya tatu, basi moja ifungwe.

Unafanyaje mlalahoi wewe katika mtihani huo, tukajikuta tunaomba po! Tukamwomba mhudumu atufungie tutajua nini cha kufanya maadam tuna majokofu vyumbani.

Lakini kwa kuwa 'ladies first', tukamwachia bibie ili aende naye chumbani atajua jinsi ya kumshughulikia Chimaek wake.

Siku nyingine tukaamua tujitose kwenye mgahawa wa kitimoto, hapo unakuta kitimoto ya kuchoma na ya kukaanga pia, lakini na supu yake ukitaka. Astaghafirulah!

Tukadhani mchezo, nako tukaletewa jisahani limesheheni nyama na mbogamboga mbichi.

Tukaambiwa hizo mbogamboga unazitumia kuviringa mnofu na kuutafuna ili kupunguza mafuta mafuta.

Tukazoea, tukafakamia kitimoto na mbatata hadi mitumbo ndi na kujiondokea, lakini ni baada ya kushushia na Soju. Ni kinywaji kikali kilicho ndani ya chupa sawa na ya bia yenye ujazo wa miligramu 300, lakini ukipiga chupa tatu kama hujazungumza Kikorea na kuimba nyimbo za kabila lenu, basi wewe mwanamume.

Wengine siye tukabahatika kushushia na Coca Cola na Sprite. Kilichonifurahisha ni kwamba jamaa wa Korea mchana huwaoni, usiku sasa, weee utakutana nao mitaani wanayumba huku na kule kumbe Soju imeshafanya yake, hususani wazee.

Lakini, hata vijana ndio wakati unawakuta wanakamata kitimoto, kuku, samaki na mbogamboga wakiwa jozi.

Tulipodadisi, wakasema Wakorea hawapiki majumbani, wanakula sana migahawani hususan usiku na ndiyo sababu migahawa ni mingi karibu kila kona ya mji kwa kuwa mlo kwao ni sakramenti, ingawa maisha ni magumu.

Walisema maisha yakiwa magumu kwako ni magumu kwelikweli na hakuna wa kukusaidia, ndiyo sababu sisi wakawa wanatuona tunapitisha uchakavu ili kulipia tulichokula kila mmoja na kiasi cha 'won' alizokuwa nazo.

Walishangaa zaidi, mmoja wetu alipoingia mfukoni kuwanunulia Soju Wakorea tuliokuwa tumekaa nao jirani tukiwasikia wakiisifia 'Tanjania' wakikiri kusikia sifa za Mlima Kilimanjaro, nasi kwa kurejesha ukarimu ule jamaa yetu akawapiga na Soju.

Hata tulipoondoka siku hiyo kurudi kulala, walitufuatilia kwa macho mpaka tunakata kona ya kuelekea ilikokuwa hoteli yetu, kwa sababu ilikuwa ni kutembea tu kufika.

Nakumbuka onyo la "ole wako uonekane unasumbua msichana wa Kikorea, usiku huo huo utarudishwa kwenu"!

Lililonimaliza ni nilipoambiwa na jamaa yetu mmoja Mbongo anayeishi Seoul, kuwa katika familia ya Kikorea, mwanamke ana thamani kubwa akifuatiwa na mtoto, kisha mbwa na hatimaye mume. Kwa hiyo wewe kidume unapomwona mbwa hapa wa nini, ujue Korea mbwa ni bosi wako!

Halafu kumbe kutokana na wingi wa watu na udogo wa nchi ile, lakini wanaishi sana na asilimia 70 ni wazee, hivyo wanatakiwa kuzaa sana, ingawa kipato nacho mtimanyongo, hivyo mwanamke akibahatika kuzaa tu, serikali inampa dola za Marekani 100,000.

Mpe Mbongo fursa hiyo sasa! Weee!

Siku moja kabla ya kurudi Bongo, dereva wetu Paul akatupeleka mgahawa na kanisa moja hivi, kufakamia supu ya vifaranga vya kuku! We acha tu. Nitakukumbuka Korea Kusini. Tuliupiga mwingi hakika. Tutarudi tena! Inshallah!

BIASHARA

# Wakulima wa ufuta Rufiji walia kuangaliwa na bei yenye ahueni

**Na Yasmine Protace, aliyekuwa Ikwiriri**

HADI sasa nchini kuna mfumo wa ununuzi wa mazao uitwao TMX. Ni mfumo wenye orodha ya kubadilishana bidhaa nchini Tanzania.

Mabadiliko hayo ya bidhaa yamewekwa, ili kuwasaidia wakulima tofauti kupata soko bora la ndani na kimataifa, ikiwamo kupata bei nzuri katika uuzaji mazao yao.

Pamoja na kuwekwa mfumo huo na serikali kwa ajili ya kuwanufaisha wakulima, kuna baadhi ya wakulima wanadai hawautaki mfumo huo, kutokana na dai kwamba hauna sura ya kuwanufaisha na hawajui namna ya kufanya biashara tajwa.

Hivi karibuni kulifanyika Mnada wa Tatu wa zao Ufuta. Kupitia mfumo huo, wakulima wa wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, wakatoa maoni yao kwa Nipashe iliyokuwapo mahali hapo.

Kimsingi, wamezungumzia mfumo huo kuwa hauwasaidii na badala yake wanaiomba serikali irudishe mnada kwa mfumo uitwao Maboksi.

Ni kama awali ambako wanaona wanunuzi kujitokea kwa wingi kutaka kununia bidhaa kwa viwango tofautii vya fedha.

Hamis Juma, mkazi wa Ikwiriri, Rufiji anasema kuwa hawaridhiki na mnada, unaoendeshwa na mfumo wa mauzo kupitia elektoniki (TMX).

"Mfumo huo hauna uwazi ni nani anayeanzisha na kufunga mnada huo," anasema Juma, akifafanua kwamba,

uuzwaji ufuta, hadi sasa bei yake hairidhishi, ikifananishwa na mikoa mingine, bei inakuwa zaidi ya shilingi 3,000 kwa kilo moja ya ufuta.

Aisha Shabani, mkulima wa korosho, anasema kuwa mnada unatakiwa kuwajumuisha wanunuzi kutoka duniani kote na akinena kwamba, ushindani wa mnada unatakiwa.

"Hatuoni ushindani wa mnada sokoni wateja ni wachache, serikali inatakiwa ihakikishe wanunuzi angalau zaidi ya 20," anasema.

Hassan Abdu, mkulima wa ufuta anasema kuwa mfumo wa sasa mnunuzi hawamjui, pia mzigo wote hawaununui ,ikiwamo na kuchelewa kwa mnada huku wakinunua tani chache.

Anafafanua kuwa, hawautaki TMX, wanataka mfumo wa sanduku wa zamani, wakifafanua yake kwamba:

" Mfumo wa amani wa maboksi, wanunuzi wanatuma barua zinazoonyesha bei ambayo watanunua, ambao ikifika siku ya mnada, wanafungua zile barua na kuangalia bei za wanunuzi na kisha kuchagua bei ambayo wataitaka."

Zuwena Sheweji, katika nafsi yake anatafsiri kuwa mfumo mgumu, hata kuwa changamoto kwao, hawajui wanunuzi wanafanya maongezi na nani.

"Toka mnada wa kwanza hawajapata mrejesho wao wanataka maboresho ya mfumo," anasema.

Anasema mnada ujao kama maboresho hayatakuwapo,hatakubali kuendelea na mnada.

**KUTOKA CORECCU**

Mwenyekiti wa Ushirika mkoani Pwani (CORECCU), Mussa Mng'eresa, anasema wakulima wake wamepokea bei kwa ukimya.

Analinganisha tofauti mkoani Dar es Salaam, unapouzwa ufuta kwa shilingi 3570, Ikwiriri mkoani Pwani ufuta huo unakozalishwa unauzwa kwa bei ya shilingi 3000.

Anaongeza kuwa, malengo ya wakulima hayafikiwa kutokana na mfumo wa TMX na anaongeza kuwa, wakulima wanasema mfumo mbadala usipotumika hawatakubali kuuza ufuta wao.

Mussa anaitaka serikali mkoa wa Pwani kulianagalia hilo, huku yeye binfasi akitarajia kuonana na Mkuu wa Mkoa Pwani, kujadili suala hilo, ikiwezekana urekebishwe.

Anaongeza kuwa, wakulima wamemtuma suala la ufuta lifanyiwe kazi, huku Meneja wa Coreccu Mkoa Pwani, Hamis Mambawela, anasema kuwa mnada wa mkoa wa Pwani ni a tatu.

Walikuwa na tani 2750, ambazo bei ya juu ilitangazwa kuuzwa shilingi 3350 na ya chini, ilitangazwa kuuzwa shilingi 3030 huku bei ya wastani iilikuwa shilingi 3014.17.

Anafafanua ndani ya changamoto hizo, wakulima wameuza kwa shilingi 3,014.17.

**DC RUFIJI**

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji,Edward Goel amewataka wakulima kuleta ufuta katika maghala ili uuzwe.

" Changamoto zote mlizosema tunazichukua na kuzifanyia kazi. Ufuta mlete katika maghala na msiuwache nyumbani" anasema.

Anaongeza kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, atakuwa na kikao jijini Dodoma na viongozi wa vyama vya ushirika - amcos.



Mfanyakazi katika dala la mazao Ikwiriri, akiwa amebeba gunia la ufuta. **PICHA: YAMSMINE PTOTACE.**

## PROGRAMU YA RAIS INAYOMEA KWA KASI KUWANASUA WALIKO KIMKOA

Inatoka Uk 11

biashara na pia kinamama wanaomba pia kujengewa masoko ili bidhaa zao za usindikaji ziweze kuuzwa...," anasema.

**MKOANI MORO**

Nako mwezi uliopita, kukazinduliwa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Mkuu wa Mkoa akiwa mgeni rasmi, Adam Malima, anayetaja hatua muhimu kwa mkoa kuwafanya Watanzania wanahangaikia shughuli za ujasiriamali kwa tija.

"Mkoa wetu umepokea mradi huu wa Imarisha Uchumi na Mama Samia kwa mikono miwili na tunaahidi kufanya vizuri zaidi, "akasisitiza, akiamini ina nguzo ya kumkwamua mwanamke kiuwezeshaji ni mafunzo.

Anasema hadi sasa, kipaumbele cha Morogoro ni kilimo na wamejipanga kuingiza mbegu za karafuu, michikichi, kokoa na parachichi watakazozigawa bure, kama njia ya kuyawezesha makundi yaliyopo kunufaika.

Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng`i Issa anasema programu mkoani Morogoro, kuna fursa kubwa katika kilimo, kutokana na ardhi yake nzuri, yenye rutuba na watu wengi wanaoshiriki kilimo na shughuli nyinginezo za kijasiriamali.

Anafafanua, hadi sasa baraza lake linaratibu mikoa kufanya kazi ya kusaidia makundi na wanayoyaingiza katika kanzidata zao, hatimaye wanufaike na uwezeshaji utakaotolewa na programu hiyo.

Mama Issa anasema, programu hiyo imekuja kuboresha shughuli zao za kilimo na shughuli zote za kijasiriamali wanazofanya na lengo ni kuwawezesha Watanzania kuwa na maisha bora.

**JUKWAA WANAWAKE**

Katibu wa Jukwaa la Wanawake Wilaya ya Mvomero, Sebastinana Mbaga, anasema ujio wa program hiyo, inawakwamua wanawake na makundi mengine kiuchumi.

Anasema, katika wilaya yao wanafanya shughuli za kiuchumi na kijasiriamali za kilimo, kuongeza thamani mazao ya kilimo, uchuuzi na ujasiriamali mbalimbali.



# Zungu: Chakula ndiyo usalama namba moja

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Spika wa Bunge, Mussa Zungu, amesema licha ya taifa kuwa na jeshi lakini chakula ndiyo usalama namba moja, hivyo ipo haja kwa serikali kuwekeza kwenye sekta ya kilimo ili kuwa na akiba ya kutosha.

Alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua kongamano la wadau wa kilimo lililoandaliwa na Taasisi ya Uboreshaji Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT).

Alisema taifa linaweza kuwa na kila kitu ikiwamo majeshi ya ulinzi na usalama, lakini chakula ndiyo usalama namba moja hivyo wadau wa sekta hiyo wanapaswa kuweka mkazo kuiunga mkono serikali kwenye kilimo chenye tija.

"Hakuna kitu muhimu kwenye taifa kama usalama wa chakula unaweza kuwa na jeshi, mgambo lakini bila usalama wa chakula hakuna kitu" alisema Zungu.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha nia ya kulikomboa taifa kwa kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye bajeti ya kilimo, hivyo wadau pamoja na wananchi wanapaswa kumuunga mkono.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha dhamira ya dhati katika kilimo kwa kuwekeza kiasi kikubwa cha fedha hivyo wataalam wa kilimo nchini wanapaswa kumuunga mkono ili kulifanya taifa kuwa na chakula cha kutosha na kuuza nje ya nchi ziada" alisisitiza Zungu.

Alisema hivi sasa katika sekta ya kilimo wakulima wanakabiliwa na tatizo la wataalamu pamoja na masoko ya mazao ya kilimo hali ambayo inawakwamisha kufikia malengo yao.

"Wataalam wa kilimo mnapaswa kuwasaidia wakulima wetu ili kufikia malengo yao kwani hivi sasa wakulima wanakabiliwa na changamoto ya utaalamu katika kilimo lakini pia masoko ya mazao yao ya kilimo.

"Hivyo ni lazima tuone namna ya kuwapatia suluhu ya changamoto zao, duniani kote wanawekeza kwenye kilimo kwa vijana na wanawake, kwa mafano nchi ya Ethiopia walikuwa wanachukua vijana 10,000 kila mwaka kuwapeleka kwenye sekta ya kilimo na hivi sasa wanazalisha ngano kwa wingi hii yote ni kutokana na utashi wa nchi " alisema Zungu. Aidha alisema kongamano hilo litumike kwa washiriki kijifunza mbinu mbalimbali za kuongeza tija kwenye kilimo ili kuzalisha ajira. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mariam Ditopile, alisema wanaipongeza serikali kwa jitihada ambazo inafanya kwenye sekta hiyo.

"Mheshimiwa Naibu Spika sisi kama kamati tutaendelea kuisimamia wizara na kuishauri serikali ili kilimo ambacho kinategemewa na idadi kubwa ya Watanzania kiwe na tija kwao" alisema Ditopile. Ofisa Mtendaji Mkuu wa AMDT, Charles Ogutu alisema lengo la kongamano hilo ni kuhakikisha kuwa teknolojia zilizowekezwa zinawafikia wakulima kwa wakati.

Alisema: "Tutaendelea kufanya kongamano hili kila mwaka ili kuhamasisha na kuchochea ubunifu zaidi katika sekta hiyo ili kuhakikisha wakulima wananufaika".



Mkalimani wa lugha za alama (kushoto), akiwatafsiria wenye matatizo ya kutosikia kwenye eneo la wageni, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanasiasa watajwa chanzo kuzalisha hoja za CAG

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

WANASIASA wametajwa kuwa chanzo cha kusababisha kuzalishwa kwa hoja zinazoibuliwa na ukaguzi unaofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kutokana na kuingilia kanuni za manunuzi na maamuzi yanayotolewa na watendaji.

Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, Jumanne Mlagaza alisema hayo juzi katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kilicholenga kujadili hoja zilizoibuliwa na CAG katika halmashuri hiyo.

"Miongoni mwa wanaozalisha hoja mpya ni wanasiasa kuingilia maamuzi ya watendaji na kanuni za manunuzi, wanasiasa tumepewa kazi kubwa hivyo tujiepushe na kuingia jikoni," alisema.

Mlagaza alisema katika mwaka huu wa fedha atakayezalisha hoja awe mwanasiasa au mtumishi yeyote bila kujali ana cheo chochote atawajibishwa na kwamba hakuna sababu ya kuwa mafundi wa kujibu hoja, huku zikiendelea kuzalishwa nyingine.

Naye Katibu Tawala Msaidizi Usimamizi, Ufuatiliaji na Ukaguzi, Shaban Mongomongo alisema hoja nyingi zinazozalishwa kwenye halmashuri ni kutokana na uzembe wa baadhi ya watumishi kutowajibika ipasavyo katika maeneo yao.

Alisema ili kukomesha tatizo hilo la uzembe unaofanywa na baadhi ya watendaji ifike wakati wenye mamlaka wawe wanachukua hatua kwa watumishi wazembe.

Mkaguzi Mkuu ofisi ya CAG Mkoa wa Singida, Othman Jumbe, alisema endapo watendaji watakuwa wanafanya kazi kwa kufuata miongozo, sheria na kanuni hoja zitakuwa hazijitokezi.

Jumbe alisema hata hoja zinazoibuliwa na CAG kama utaratibu utakuwa unafuatwa vizuri kuzijibu zitakuwa hazijirudii kila mwaka kama ilivyo hivi sasa, ambapo hoja moja inakuwa inajitokeza karibu kila mwaka.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Annastazia Tutuba, alisema maelekezo yote yaliyotolewa na wakaguzi yatazingatiwa ili kutozalisha hoja nyingi.

# TLS yasema kifungu cha uhuru wa kujieleza kina tatizo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAKAMU wa Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Deus Nyabiri amesema kuna ulazima wa kuifanyia marekebisho Katiba ya nchi ili iendane na sayansi na teknolojia ya sasa, hususani kwenye kifungu cha uhuru wa kujieleza.

Nyabiri alisema hayo wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo mawakili kuhusu uhuru wa kujieleza jijini Dodoma.

Mwanasheria huyo mwandamizi alisema kila mtu duniani ana uhuru wa kujieleza tangu anapozaliwa na hata Katiba ya nchi imelieleza hilo, lakini kwa sasa kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia kuna haja ya kufanyia marekebisho sheria inayohusu uhuru huo na hata ikibidi katiba yote.

"Katiba imeeleza vizuri kuhusu uhuru wa kujieleza lakini pia hata na mipaka ya uhuru huo kuwa usivunje sheria za nchi lakini kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yaliyopo ambayo yanavunja mipaka iliyowekwa kwenye Katiba kuna haja ya kuangalia upya vifungu vyake pamoja na sheria zilizopo," alisema.

Alisema kuwa kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yaliyopo duniani kila mtu anatumia uhuru wa kujieleza kwenye mitandao ya kijamii kama anavyotaka bila kujali kama anavuka mipaka iliyowekwa au la au, hata kama anawaudhi watu wengine kuhusu uhuru huo.

Alisema hata Sheria ya Makosa ya Mtandaoni iliyopo inawabana wale ambao wanatumia mitandao ya kijamii vibaya na kuwaachia wale ambao wanatumia uhuru wao wa kujieleza kwa kuwadhalilisha wengine mitaani, bila kutumia mitandao na kutaka sheria hiyo sasa iwabane watu wote bila kujali wanatumia mitandao au la.

Naye, Esta Safari kutoka mkoani Mwanza alisema hata wateja wanao wahudumia hawajui mipaka ya kujieleza inaishia wapi kwani wengi wao ni wale ambao wanatumia mitandao ya kijamii kuelezea fikra zao.

Alisema wengi hawajui kama kuelezea fikra zako mitandaoni kunaweza kuleta taharuki kwa watu wengine kwa kuvunja amani au kuhatarisha usalama wa nchi, hivyo huwa wanajikuta wakiangukia kwenye vyombo vya sheria bila kujua.

Alisema kuwa ili suala la uhuru wa kujieleza likae vizuri ni lazima mabadiliko yaanzie kwenye Katiba na sheria zilizopo, kwamba watu wengi wanajikuta wamevunja mipaka bila kujua hasa kwa kutumia mitandao ya kijamii kwa kudhani kuwa ni haki yao kumbe kuna mipaka ambayo hawapaswi kuvuka hata kama wanajieleza.

Wakili Ferdinand Makore alisema kuwa japo Katiba imeeleza kuwa kila mtu ana uhuru wa kujieleza na kuweka mipaka ya uhuru huo lakini kuna haja ya kuangalia upya mipaka hiyo kutokana na mageuzi ya teknolojia iliyopo sasa.





# Wakulima pareto wazitilia shaka maabara za wanunuzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa pareto katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kuweka utaratibu mzuri wa uendeshaji wa maabara za wanunuzi wa zao hilo, wakidai kuwa kuna mchezo mchafu unafanywa na wanunuzi.

Wakulima wa zao hilo katika kata za Santilya na Itawa waliwasilisha ombi hilo juzi kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Beno Malisa alipofanya ziara ya kusikiliza kero za wakulima, ambapo walisema maabara hizo zinafanya kazi kwa kificho. Mmoja wa wakulima hao, Cosmas Sishamba alisema wanunuzi wa pareto wanachukua sampuli na kwenda kupima kiwango cha sumu bila kuwa na uwakilishi wa wakulima na kuwaletea majibu kuhusu kile kilichobainika na kupanga bei. Alisema hali hiyo inawapa wasiwasi kwamba huenda kile kinachobainika kwenye pareto hiyo ni tofauti na uhalisia na hivyo wanunuzi wakawa wanazitumia kuwapunja wakulima.

Aliomba serikali kuwaweka wataalamu wake kwenye maabara hizo ili wao ndiyo wasimamie badala ya kuwaachia wanunuzi kumiliki maabara na kupanga bei wao wenyewe.

"Mnunuzi anamiliki yeye mwenyewe maabara, anakwenda kupima kiwango cha sumu na kututajia bei kulingana na alichokiona kwenye pareto bila sisi wakulima ama serikali kushiriki, sasa tutapataje haki? Tunaomba serikali iwatumie wataalamu ambao imewasomesha ndiyo wasimamie maabara hizi," alisema Sishamba.

Naye Philemon Wilias alisema miaka ya nyuma wakulima walikuwa wanashirikishwa kwenye vikao mbalimbali vya wadau wa zao hilo vikiwamo vinavyotumika kupanga bei lakini kwa sasa hawashirikishwi na badala yake wanalazimika kuuza kwa bei waliyopangiwa.

Alisema kwa sasa baadhi ya watu wanaoshiriki kwenye vikao na mikutano ya wadau wa pareto hawana ujuzi wowote na wala hawajui chochote kuhusu uzalishaji wa zao hilo na hivyo akaomba utaratibu wa kuwashirikisha wakulima urejeshwe.

Mkuu wa Idara ya Kilimo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda, alisema miaka ya nyuma kampuni za kununua pareto zilikuwa mbili pekee hali ambayo ilikuwa inasababisha ushindani wa bei kuwa mdogo. Alisema wakati huo kilo moja ya pareto ilikuwa inanunuliwa kwa Sh. 2,000 lakini kwa sasa kampuni zilizosajiliwa zimefika sita na ushindani wa bei umeongezeka hali iliyosababisha bei kupanda mpaka Sh. 3,500 kwa kilo moja.

Hivyo, aliwataka wakulima kuendelea kufuata taratibu mbalimbali za uzalishaji wa zao hilo wanazofundishwa na wataalamu ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kukuza uchumi wao. Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Malisa alisema serikali imeshaanzisha utaratibu wa kudhibiti uendeshaji wa maabara za kupima sumu ya pareto kwa kuanzisha siku maalumu ya kupima badala ya kila mnunuzi kupima kwa muda wake.

Vilevile alisema kwenye kila maabara kuna maofisa wa serikali ambao wanafanya kazi ya kuhakiki upimaji wa sumu hiyo ili kuzuia wanunuzi hao kuwapunja wakulima kwa kutoa matokeo tofauti na uhalisia.



Wakulima wa pareto wa Kata ya Santilya, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakimsikiliza Mkuu wa Wilaya hiyo, Beno Malisa (hayupo pichani), alipofanya ziara ya kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili kwenye kilimo cha zao hilo, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mradi wa umeme Tabora- Katavi kukamilika mwaka huu

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

MRADI mkubwa wa umeme wa Tabora-Katavi unaojengwa na kampuni ya kusambaza na kusafirisha umeme (ETDCO), ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme nchini (Tanesco), unatarajiwa kukamilika mwaka huu.

Kukamilika kwa mradi huo wa msongo wa kilovolti 132 kutaondoa changamoto ya umeme kwenye Mkoa wa Katavi.

Kaimu Meneja Mkuu Kampuni ya ETDCO, Sadock Mugendi, alisema jana kuwa wanaendelea kujenga miundombinu ya umeme kwenda Katavi kwa kasi ambayo itawawezesha kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Alisema lengo la mradi huo wa kimkakati ni kuhakikisha Mkoa wa Katavi kuunganishwa na gridi ya taifa ili mkoa huo uwe na umeme wa uhakika.

Mugendi alisema ETDCO imekuwa suluhisho la miundombinu ya umeme kwani tangu kuanzishwa mwaka 2016 imefanikisha kusambaza umeme kwenye mikoa mbalimbali nchini. Alisema mradi wa kutoka Tabora kwenda Katavi (km383) ambao unatarajiwa kumalizika mwaka huu utasababisha umeme wa uhakika mkoani Katavi. Alisema kukamilika kwa mradi huo kutaipunguzia gharama TANESCO za kununua mafuta ya dizeli kwa ajili ya jenereta linalotumika kuzalisha umeme kwenye Mkoa wa Katavi.

Aidha, aliipongeza serikali kwa kuendelea kuwekeza kwenye sekta ya nishati akisema hali ambayo imeiwezesha mikoa mingi nchini kuwa na umeme wa uhakika hata maeneo ya vijijini.

Alisema ETDCO imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya umeme nchini na kwamba imesaidia kuondoa changamoto ya nishati hiyo ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa Uchumi.

Alisema wanatekeleza miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) ambayo iko katika hatua mbalimbali na mingi imekamilika na wananchi wanapata umeme wa uhakika.

Alisema ETDCO inaunganisha umeme kwenye nyumba 5,000 Msomera Handeni Tanga na mpaka Julai mradi huo utakamilika na kwamba wanajenga mradi mwingine wa miundombinu ya umeme kutoka Arusha kwenda kituo kidogo Njiro kuimarisha upatikanaji wa umeme mkoani humo.

Alisema mkoani Mbeya wanatekeleza mradi mwingine wa kimkakati wa REA ambao umefika asilimia 90.

# Njombe yashindwa kufika lengo ukusanyaji mapato

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KATIBU Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, amesema kuna upungufu kwenye ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, kwamba kati ya makadirio ya Sh. bilioni tano zimekusanywa Sh. bilioni nne.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Madiwani cha kujadili hoja za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kilichofanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Alisema kuwa upungufu huo umeonekana kwenye ushuru na kodi ya huduma ambapo asilimia 30 ya mapato hadi sasa haijakusanywa ambayo ni sawa na Sh. bilioni moja. "Kwenye usimamizi wa mapato kwenye halmashauri bado kuna changamoto, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mpaka sasa hadi Mei mwishoni imefikia asilimia 70 ya makusanyo yaliyopangwa kwa mwaka huu 2023/24 kiwango bado kiko chini," alisema Omari.

Pia aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa maamuzi ya kuhamia ofisi ya makao makuu baada ya jengo lao kukamilika na kwamba kwa kufanya hivyo itasaidia kutoa huduma kwa haraka kwa wananchi.

Mkurugenzi wa Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Christopher Sanga, alisema halmashauri hiyo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watumishi katika kada mbalimbali.

Alisema halmashauri ilikuwa na hoja 12 sawa na asilimia 41.4 ambazo zimehakikiwa na mkaguzi na kufungwa, hoja 17 sawa na asilimia 58.6 zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali Mkoa wa Njombe, Willy Ondule, alishauri kufutwa kwa hoja za muda mrefu pamoja na kuacha kuzalisha hoja ambazo siyo za msingi.



# Makamu wa Rais: Utalii utamaliza tatizo ukosefu wa ajira

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kuelekezwa juhudi zaidi katika suala la uchumi kwenye sekta ya utalii Zanzibar kunatoa fursa katika kusaidia nchi kukukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira nchini.

Aliyasema hayo juzi Nungwi Kaskazini 'A' Unguja alipokutana na wamiliki na viongozi wa mabwawa ya kufugia kasa na wanyama wa asili katika eneo la Mnarani Nungwi.

Alisema kunapokuwapo fursa ya kiuchumi kama hiyo ya sekta ya utalii mtazamo wa serikali na viongozi ni kwamba kwanza kufaidika vyema wananchi kiuchumi kulingana na uwezo wao.

Kadhalika alisema kutokana na jitihada zinazooneshwa na wanachi serikali inawajibu pia kushirikiana nao katika kutengeneza miundombinu ili mwananchi wa kawaida aweze kufaidika na fursa hiyo.

Alisema huduma kama hizo za ufugaji wa wanyama pamoja na kasa zinatolewa katika nchi nyengine duniani, lakini kinachohitajika ni wananchi kuwezeshwa ili shughuli hizo kufanyika kwa umahiri na maarifa makubwa.

Hivyo, aliwashauri wadau hao kuhakikisha kwamba wanashirikiana vyema na serikali kusaidia kuweka mazingira rafiki ya kuendeleza shughuli hizo kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vinavyohitajika.

Pia, aliwataka wadau hao kujiimarisha, kuendelea kuangalia fursa nyingine za ziada zilizopo na wanapozibaini ni wajibu wa wadau hao kushauriana na serikali ili kuona namna gani watapata msaada.

Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Othman Ali Maulid, alisema wilaya hiyo ina hoteli za utalii 270 na kati ya hizo 17 ni za nyota tano.

Alisema mapato yote ya utalii kulingana na takwimu zilizopo ni kwamba Mkoa wa Kaskazini Unguja pekee unachangia zaidi ya asilimia 60.

# Serikali yafafanua lengo la marekebisho sheria ndogo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema marekebisho ya sheria ndogo yaliyopitishwa na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi yamelenga kuviwezesha vikosi vya idara maalum kuleta ufanisi, kufanya kazi za uzalishaji na biashara katika miradi na kuongeza mapato.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji, wakati akijibu hoja za wajumbe wa baraza hilo waliochangia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali uliowasilishwa mbele ya baraza hilo.

Alisema serikali imefanya marekebisho makubwa katika idara maalum za serikali katika vikosi vyake ikiwamo Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) pamoja na Kikosi cha Valantia kwa lengo la kuleta ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yake.

Alisema katika marekebisho hayo vikosi hivyo sasa vimepewa uwezo wa kufanya kazi za uzalishaji mali na ujasiriamali kwa ajili ya kuongeza mapato na kujiendesha kwa ufanisi.

Aidha, aisema katika kipindi cha miaka mitatu sasa vikosi hivyo vimeonesha uwezo mkubwa pamoja na kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi wa masoko, hospitali pamoja na shule za ghorofa za sekondari Unguja na Pemba.

''Mheshimiwa marekebisho ya sheria ndogo sasa yatavipa uwezo vikosi vyetu kufanya shughuli za uzalishaji na biashara katika miradi hatua ambayo itasaidia kuongeza mapato pamoja na wapiganaji wetu kupata ujuzi wa kazi za mikono,'' alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi viongozi wakuu wa kitaifa, Machano Othman Said, alipongeza marekebisho hayo ya sheria ambayo sasa yatavipa uwezo vikosi hivyo kutekeleza majukumu yake katika mwelekeo wa biashara na uzalishaji mali.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum, Masoud Ali Mohamed, alisema katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi mageuzi makubwa yamefanyika katika vikosi ikiwamo kuviwezesha kutekeleza majukumu yake ya kazi za ujasiriamali.

Alisema vikosi hivyo vimejenga majengo ya kisasa katika masoko yote ya Unguja na Pemba kwa viwango na vigezo vinavyokubalika.

Alisema kutokana na mageuzi hayo marekebisho ya sheria yanahitajika ambapo yatavipa uwezo wa kisheria vikosi hivyo kufanya kazi za utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kiuchumi na kuongeza kipato.




Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria Wizara ya Katiba na Sheria Zanzibar, Hanifa Ramadhan Said, akizungumza katika kongamano la vyuo vikuu la masuala ya msaada wa kisheria, huko Tunguu, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wananchi wahimizwa kutumia vituo vya msaada kisheria

**Na Mwandishi Wetu**

JAJI wa Mahakama Kuu Zanzibar, Ibrahim Mzee Ibrahim, amewataka wananchi kuvitumia vituo vya msaada wa kisheria katika maeneo yao ili kupunguza gharama na kufuata huduma hiyo mbali.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua kongamano la vyuo vikuu la masuala ya msaada wa kisheria Zanzibar.

Alisema lengo la serikali kuanzisha vituo hivyo ni kuwaondoshea usumbufu huo na kuitaka jamii kuvitumia ipasavyo ili kufikia malengo yaliokusudiwa.

"Kabla ya kuwepo wasaidizi wa sheria katika jamii watu wengi walikosa msaada wa kisheria jambo ambalo lilisababisha kukosa haki zao," alisema Jaji Ibrahim.

Alisema msaada wa kisheria ni muhimu katika jamii na baadhi ya watu hawana uwezo wa kulipia mawakili, hivyo msaada wa kisheria utawajengea ujasiri wa kupambania haki hizo.

Aidha, aliipongeza idara ya katiba na msaada wa kisheria kuandaa kongamano hilo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu ambapo litasaidia kuhamasisha upatikanaji wa huduma katika ngazi ya jamii na vyuo vikuu.

Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria Zanzibar, Hanifa Ramadhan Said alisema madhumuni ya kongamano hilo ni kuwajengea uzalendo, kujitolea na kuisaidia jamii kupitia msaada wa kisheria.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kuwaunga mkono katika shughuli mbalimbali zilizoandaliwa na idara hiyo katika wiki ya msaada wa kisheria hadi kufikia kilele chake Juni 28.

Hata hivyo, aliwapongeza wadau wa maendeleo wakiwamo Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Taasisi ya Msaada wa Kisheria (LSF) kwa kuwaunga mkono na kuhakikisha jamii inapata haki zao kupitia msaada wa kisheria.

Mratibu na Mshauri wa Programu za Utawala Bora wa UNDP, Godfrey Mulisa, alisema shirika hilo litaendelea kuisaidia serikali kupitia idara ya katiba na msaada wa kisheria katika mambo mbalimbali ikiwamo kutoa elimu ya msaada wa kisheria ili wananchi wapate stahiki zao.


Mkuu wa Shule ya Sheria Zanzibar, Dk. Ali Ahmed Uki na Kaimu Mkuu wa Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZU), Dk. Sikujua Omar Hamdan, walisema uwepo kwa vituo vya msaada wa kisheria vyuoni kunasaidia kujenga weledi na uzoefu kwa wanafunzi wa kada ya sheria kuweza kuisoma kwa vitendo fani hiyo.

Aidha, alisema hali hiyo pia itaweza kuwajengea moyo wa kuitumika jamii kwa kujitolea hata baada ya kumaliza masomo na kuwataka wanafunzi wanaotoa msaada wa kisheria chuoni wasivunjike moyo.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL EZRA BWERE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S2499/0609 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia TUSIIME SECONDARY SCHOOL mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/127147/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DORICAS WENCESLAUS ISHENGOMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye usajili namba **T 162 DLW.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/109932/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANCISKA VON HELAND**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER PRADO** Yenye usajili namba **T 203 CD 763.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taaifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/127463/2024**


**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU**
**Shauri la Ndoa Na 37/2024**
**Jina la mdai RACHEL DAVID**
**Jina la mdaiwa ROBERT SILYVESTER**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**( Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa :**
**ROBERT SILYVESTER**
**WA MWATULOLE**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za madai)**
**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 10 mwezi 07 mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo .

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 mwezi 07 mwaka 2024




**NOTICE OF DATE OF HEARING TO APPELLANT AND RESPONDENT**
**IN THE DISTRICT COURT OF CHUNYA**
**AT CHUNYA**
**MATRIMONIAL REVISION NO. 11206 OF 2024**
**ORIGINAL Matrimonial Case No. 19 of 2022**
**Of the primary court of Chunya District at MAKONGOLOSI**
**Appellant WITNESS MBEYANJE**
**Versus**
**Respondent FESTO NSELLA**

**TO: FESTO NSELLA**
**POPOTE ALIPO**

Take notice that the above mentioned appeal has been fixed for mention/ hearing on the 10th Day of July 2024 and you are required to enter appearance at such time and date.

AND TAKE FUTURE NOTICE THAT, If you default to enter appearance as aforesaid in the appeal and he determined us your absence.

Given under my hand and the seal of the Court this 25th day of JUNE 2024




## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**ABBAS HASSANI SABUNI**

anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya FEKON zenye usajili namba MC 840 AND na MC 936 ALX, CHASSIS NAMBA : LDAPAJOB9EGB06939 na LDAPAJOB8EGB11842 na ENGINE NAMBA: 157FM1214F07169 na 157FM1214F11842. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/TAN/MUH/6338/2024**

## KUPOTEA KWA PIKIPIKI

**MWAJUMA ABDALLAH ISSA** anatangaza kupotea kwa pikipiki aina ya FEKON yenye usajili namba T 904 BYY , CHASSIS NAMBA: LDAPAJ0B1BGB18692 na ENGINE NAMBA: 157FMI211152893. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/TAN/MUH/6421/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ALES PAUL BWANAKUNU** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya BOXER na TVS zenye usajili namba ; MC 983 CRM, MC275 CRP, MC 974 CTN, MC 347 CVB, MC 349 CVB, MC 352 CVB, MC 357 CVB, MC 359 CVB, MC 851 CYB, MC 911 CZE, MC 384 DBZ, MC 400 DBZ, MC 791 DEJ, MC 515 DEL, MC 577 DNV, MC 578 DNV, MC 579 DNV, MC 581 DNV, MC 118 DPM, MC 120 DPM, MC 122 DPM, MC 124 DPM, MC 126 DPM na MC 562 DQG. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/128436/2024**
**PHQ/DAR/KIN/128453/2024**
**PHQ/DAR/KIN/128438/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ALES PAUL BWANAKUNU** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya BOXER na TVS zenye usajili namba ; MC 721 BQX, MC 114 BQY, MC 636 CFF, MC 723 CFF, MC 389 CGC, MC 125 CHH, MC 138 CHH, MC 139 CHH, MC 484 CHP, MC 500 CHP, MC 823 CHS, MC 877 CHS, MC 853 CHX, MC 912 CHX, MC 203 CKH, MC 986 CLE, MC 987 CLE, MC 988 CLE, MC 503 CLY, MC 138 CMM, MC 140 CMM, MC 143 CMM, MC 921 CQC na MC 173 CQW. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**PHQ/DAR/KIN/128436/2024**
**PHQ/DAR/KIN/128453/2024**
**PHQ/DAR/KIN/128438/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Ndugu WARDA OMAR SALIM** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya HUONIAO yenye usajili MC 534 CCJ, kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu nawe.

Taarifa Polisi:

**PHQ/TAN/TAN/6308/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**DEED POLL**
**CHANGE OF NAME**
**(Made as per registration of documents Act CAP. 117)**

BY THIS DEED, MARIAM YAHAYA MOHAMED of KIGAMBONI – DAR ES SALAAM Do hereby verify that the two names MARIAM YAHAYA MOHAMED and MARIAM YAHYA MAYO are my true names which have used interchangeably

- That the other name MARIAM YAHYA MAYO has also been formally used as it appears in National Identity card number 1999012-41209-00001-16
- That I have formally used the name MARIAM YAHAYA MOHAMED in my Birth certificate number B/00067881

The reason of the name change is a difference of names in my National Identity Card and birth certificate. Mariam Yahaya Mohamed is my proper and legal name appeared as birth certificate. Im my other document my name appeared as Mariam yahya mayo this is a typing error that changes my name completely and create difficulties. With this document I denounce those names of Mariam yahya mayo as not my names and thereafter annaounce the names of Mariam Yahaya Mohamed as my proper name and yahaya is my father, Mohamed is my grandfather and mayo is my surname.

BY THIS DEED POLL MARIAM YAHAYA MOHAMED, HEREBY absolutely renounce and abandon that names of MARIAM YAHYA MAYO in that pursuance of such change of name as aforesaid I declare that I will be known at all times hereunder in all actions and proceedings in dealings and transactions and upo all occasions whatsoever use and sign the name of MARIAM YAHAYA MOHAMED, as my name in lieu of MARIAM YAHYA MAYO.

I FURTHER DECLARE that all transactions, certificates, deeds and commitments that I have done in the past by using my former names of MARIAM YAHYA MAYO are valid

AND DO GEREBY authorize and request all persons to designate, describe and address me as by my assumed name of MARIAM YAHAYA MOHAMED in witness wherefore, I have hereunto set my hand this 24 day of 05 2024





## KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**EFRAIMU MTIANA** anatangaza kupotelewa na nyaraka umiliki Kiwanja namba 600 Kitalu "EE" Kilichopo Ngokolo Manispaa ya Shinyanga

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu.

TAARIFA YA POLISI:**PHQ/SHI/SHI/4757/2024.**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 0677020701**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Vijana Gen-Z wazidi kuitikisa Kenya

## • Usalama wa Taifa walaumiwa...



**NAIROBI,** Kenya

MITAA mbalimbali katika jiji la Nairobi nchini Kenya, jana ilitawaliwa na milio ya milipuko ya mabomu ya machozi na risasi wakati wa makabiliano kati ya waandamanaji na vikosi vya usalama.

Waandamanaji vijana wanaofahamika kama 'Gen-Z' wameendelea kuingia mitaani kuandamana, licha ya Rais William Ruto, kukubaliana na madai yao na kuacha kuusaini muswada wa fedha wa 2024.

Kuna idadi kubwa ya vikosi vya usalama polisi, wanajeshi na maofisa usalama walikuwa katika maeneo mbalimbali ya jiji hilo wakipambana na waandamanaji hao.

Kuanzia majira ya asubuhi, barabara kubwa ikiwamo ile ya kuelekea Ikulu ya rais, zilifungwa na huku shughuli katika majengo muhimu zilisimama.

Katika maandamano yaliyofanyika siku tatu zilizopita, watu 22 wameripotiwa kupoteza maisha na idadi kubwa wakijeruhiwa.

Katika maandamano hayo yalijojaa vurugu, waandamanaji walivamia jengo la bunge na kuchoma moto.

Siku iliyofuata, Rais William Ruto alikubali shinikizo la vijana hao na kusema kwamba ataondoa muswada wa fedha ulio na mapendekezo ya kuongeza kodi na kuahidi kukutana nao ndani ya wiki nne kwa ajili ya mazungumzo.

Hata hivyo, hilo halikuwaridhisha kundi hilo la vijana na kuapa wataendelea na maandamano yao kwa kuelekea Ikulu.

Barabara zinazoelekea kwenye viunga vya Ikulu ya Kenya zimefungwa, huku wanausalama wakiwazuia baadhi ya madereva na



watembea miguu.

Pia kumekuwa na maandamano katika miji mingine nchini humo ikiwamo Mombasa, ambalo ni jiji la pili kwa ukubwa.

„Ruto lazima aende", walisikika wakiimba vijana hao wakati wakiandamana.

Mji ambao ndio ngome ya Rais Ruto wa Eldoret, ulikuwa tulivu, lakini kuliripotiwa mapigano katika mji wa Magharibi wa Migori.

### CHIMBUKO LA GEN-Z

Hakuna anayejua vizuri chimbuko halisi la vuguvugu la vijana wanaoandamana nchini Kenya, wanaojiita Gen-Z, wakimaanisha vijana wa kizazi cha sasa.

Hata hivyo, kulingana na vyanzo vinaeleza vuguvugu hilo lilianzia katika mitandao ya kijamii, hasa Tik Tok na ndiko jina hilo lilipoanzia kabla ya kuwa maarufu.

Ubunifu wa vijana hao katika kuhamasisha maandamano na kutekeleza dhamira yao, imekuwa kaa la moto linaloendelea kuwahangaisha maofisa usalama wa nchi hiyo.

Generation Z haina viongozi wakuu, badala yake inaendeshwa na vijana waliozaliwa kuanzia miaka ya 2000, na inakuwa vigumu vyombo vya dola kuwafikia.

Kutokana na wengi wao kuwa vijana wasomi na wenye uelewa, wamefaulu kutumia teknolojia ya kidijitali vizuri kwani kuanzia kupanga na maamuzi ya kuandamana yanafanyika katika mitandao ya kijamii.

Hata hivyo kwa wiki nzima, maandamano hayo yameitikisa serikali ya William Ruto, kiasi ambacho iliamua kusalimu amri na kufuata kile ambacho vijana hao wanataka.

### KUHUSISHWA KISIASA

Awali, Rais Ruto katika hotuba yake aliyoitoa Jumanne usiku, alisema maandamano hayo ya vijana yalitekwa na watu wengine ambao walikuwa na ajenda za uhaini.

Aliahidi kuchukua hatua kali endapo maandamano hayo yataendelea.

Hata hivyo katika hotuba yake ya juzi, alionekana kuwa mtulivu zaidi na kukubaliana na madai ya waandamanaji hao kwa kukataa kusaini muswada wa fedha unaopingwa

Kutokana na kuwepo utitiri wa kodi.

### USALAMA WA TAIFA

Chombo ambacho kwa sasa kinalaumiwa kutokana na kuimarika kwa ushawishi wa Gen-Z nchini humo ni Idara ya Usalama wa Taifa ya Kenya, ikielezwa kushindwa kutoa taarifa za kweli kwa kiongozi wa nchi hiyo.

Akizungumzia hilo, Naibu Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua, alinyooshea kidole Idara ya Usalama wa Taifa kuwa imeshindwa kumshauri rais hali iliyosababishia maafa nchini humo.

Gachagua alimtaka ofisa wa kitengo hicho Nurdin Haji, kujiuzulu na kuwajibishwa kutokana hali iliyotokea mpaka kuibuka kwa maandamano ya kupinga muswada wa fedha wa mwaka 2024.

Kiongozi huyo alisisitiza kwamba idara hiyo haikumpa rais ushauri kuhusu kinachoendelea na muafaka kuwa Wakenya hawakuutaka muswada huo wa fedha.

Katika hotuba yake aliyoitoa moja kwa moja kupitia Televisheni ya kitaifa, naibu rais huyo alisema vifo vya raia, uharibifu wa mali na hata uvamizi wa taasisi muhimu za serikali vingeepukika iwapo rais angelipata ushauri na taarifa za uhakika kutoka kwa idara ya intelijensia.

Alimtaka Haji kuwajibika kwa kuliangusha taifa hilo kwa kutofanya kazi yake ipasavyo.

Makamu huyo wa rais, alimshauri Rais Ruto kuunda Idara ya Usalama wa Taifa imara pamoja na viongozi wa intelijensia wanaoweza kutathimini hali kwa haraka na kumfahamisha kile kinachoendelea nchini.



# JKU SC wajipanga Kagame Cup 2024

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, JKU SC wameanza mikakati ya kujiandaa na michuano ya Kombe la Kagame inayotarajiwa kufanyika kuanzia Julai 10 hadi 28, mwaka huu jijini Dar es salaam na Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa mabingwa hao, Salum Ali Haji, alisema baada ya kufanikiwa katika Ligi kuu ya Zanzibar sasa wanaelekeza nguvu zao katika michuano hiyo ya Afrika mashariki na Kati.

**Alisema michuano hiyo itawasaidia kwa kiasi kikubwa kujiandaa vizuri kuelekea michuano ya Klabu bingwa Afrika (CAF) wao wakiwa ndio wawakilishi pekee wa Zanzibar Alisema kuelekea michuano hiyo ya Kagame anatarajia kuwa na ingizo jipya la wachezaji saba ambao malengo yao kuwatumia katika msimu mpya wa Ligi kuu ya Zanzibar na michuano iliyopo mbele yao.**

Alisema tayari kama kocha ameshawasilisha mapendekezo yake kwa uongozi wa timu hiyo aina na nafasi za wachezaji ambao watatungana na timu hiyo kwa msimu ujao.

"Tunarudi tena uwanjani baada ya mapumziko mafupi, tunafanya maandalizi kwa ajili ya mashindano yaliyopo mbele yetu yaani Kagame Cup lakini pia Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu ya Zanzibar, pia tutatumia michuano hii kuwaangalia kwa karibu wachezaji wapya ambao tunampango wa kuwasajili"alisema Ali Haji.

Alisema wataanza maandalizi yao rasmi kesho Jumamosi kujiandaa na michuano hiyo.

# YANGA YAANZA MAZUNGUMZO KUWABAKISHA MSHERY, KIBWANA

**Na Faustine Feliciane**

WACHEZAJI wazawa, golikipa Abdultwalib Mshery na Kibwana Shomari ambao wamemaliza mikataba yao na Yanga, tayari wameanza mazungumzo kwa lengo la kubaki klabuni hapo.

Nyota hao wa zamani wa Mtibwa Sugar, wote wamemaliza mikataba yao na kwa sasa ni wachezaji huru huku Meneja wao, George Job akikiri kuwapo kwa hofa kutoka klabu nyingine zikiwahitaji.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Job alisema nyota hao ambao kwa sasa wapo mapumzikoni ni wachezaji huru lakini tayari mazungumzo na klabu yao ya Yanga yameanza.

„Bado hawajasaini sehemu yoyote, wapo mapumziko, lakini ni kweli kuna ofa zimekuja ingawa pia mazungumzo na waajili wake yanaendelea,“ alisema Job.

Aidha, alisema mambo yote yakiwa sawa watatoa taarifa juu ya nyota hao kama wanabaki Yanga au kuna mabadiliko mengine kuelekea msimu ujao.

„Kwa sasa wachezaji wamepumzika, kulikuwa na matukio mengi baada ya kumalizika ligi, kulikuwa na michezo ya hisani ambayo wachezaji wangu wameshiriki kule Mbeya na Morogoro, mambo yakikaa sawa watu watajua nini kinaendelea,“ alisema Job.

Kuhusu beki wa kati, Dickson Job ambaye pia anamsimamia, alisema nyota huyo bado ana mkataba wa mwaka mmoja ndani ya timu hiyo.

**WAVU...**



Mchezaji wa Mpira wa Wavu wa Shule ya Sekondari ya Ukonga, Hasssan Jadi akiruka juu kupiga mpira kurudisha kwa wapinzaji wao Shule ya Sekondari Kiwalani jana, wakati walipokuwa wakicheza mechi maalum ya kupata timu ya Mkoa wa Dar es Salaam itakayoshiriki michuano ya Umiseta hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MASHUJAA FC YABADILISHA JINA TIMU YA WANAWAKE

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mashujaa FC imetangaza kubadilisha jina la timu yao ya wanawake ambapo sasa itaitwa Mashujaa Queens badala ya Amani Queens.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, imesema jina hilo jipya litaanza kutumika msimu ujao wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL).

Klabu hiyo yenye maskani yake Kigoma, iliinunua Amani Queens iliyokuwa na maskani yake mkoani Lindi na kuiongoza kushiriki Ligi Kuu msimu uliomalizika ikitumia jina la Amani Queens.

„Uongozi wa Klabu ya Mashujaa, unapenda kuutangazia umma mabadiliko ya jina la timu yetu ya wanawake kutoka Amani Queens, sasa itatambulika kama Mashujaa Queens kuanzia msimu ujao wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Nia na malengo ya kubadili jina hilo ni kuiunganisha timu na mashabiki pamoja na wananchi wote wa Kigoma.

Taratibu zote za usajili wa jina hilo tayari zimekamilika kwa kufuata miongozo, kanuni na taratibu zote za Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), na Baraza la Michezo la Taifa (BMT),“ ilisema taarifa hiyo.

Awali, Amani Queens ilikuwa kwenye wakati mgumu kifedha hasa ilipokuwa ikishiriki Ligi Kuu mwaka juzi kabla ya wamiliki wake kuipiga bei ambapo sasa inamilikiwa na Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ), ambalo pia linaimiliki timu ya soka ya wanaume ya Mashujaa FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara na msimu ulioisha ilimaliza kwenye nafasi ya nane kwa kukusanya pointi 35.

## ZISIKUPITE

### ZIRKZEE AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United inatazamia kukidhi kipengele cha kuachiliwa kwa Joshua Zirkzee huku wakipanga kumuuza Mason Greenwood ili kufadhili mpango huo, nao Everton wakitakiwa kuwasilisha ombi jingine kwa Jarrad Branthwaite.***(Mail)***

### BRANTHWAITE KITAELEWEKA

KLABU ya Everton inatarajia Manchester United itawasilisha ofa nyingine kwa beki wa England, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21. ***(Liverpool Echo)***

### NDIAYE ANUKIA EVERTON

EVERTON inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Senegal, Iliman Ndiaye, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Marseille ya Ufaransa. ***(Footmercato)***

### TEN HAG MKATABA WANUKIA

MANCHESTER United inatarajia kukubaliana mkataba mpya na kocha wake, Erik ten Hag, kabla ya kuanza kwa ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya ambapo wanatarajia kwenda Marekani mwezi ujao. ***(ESPN)***

### NISTERLROOY KUREJEA UNITED

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy, mwenye umri wa miaka 47, amefanya mazungumzo chanya kuhusu kurejea katika klabu hiyo kama sehemu ya wasaidizi wa Erik Ten Hag. ***(Talksport)***

### JOSELU KUONDOKA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Joselu, mwenye umri wa miaka 34, anakaribia kuondoka Real Madrid baada ya kupokea ofa kutoka kwa klabu ya Qatar Al Gharafa. ***(Athletic)***

### CHELSEA YAMFUATA GUIU

CHELSEA imeanza mazungumzo na Barcelona kuhusu mkataba wa kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Hispania, Marc Guiu, mwenye umri wa miaka 18. ***(ESPN)***

### GRAY ATAKIWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inavutiwa na kiungo wa kati wa Leeds United, Archie Gray, mwenye umri wa miaka 18. ***(Bild)***

### SPURS, CHELSEA VITANI

KLABU ya Tottenham Hotspur imeanza mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa Lille na Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David, mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia anahusishwa na kuhamia Chelsea. ***(Football Insider)***


### KUDUS NJIA MOJA

MCHEZAJI wa Timu ya Taifa ya Ghana, Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 23, amekuwa akihusishwa anajiandaa kuondoka West Ham lakini klabu hiyo bado haijapokea ofa ya kiungo huyo mshambuliaji. ***(Sky Germany)***

### NAPOLI KUMUUZA OSIMHEN

KLABU ya Napoli itazingatia ofa ya kiwango cha euro milioni 100 kwa straika wa Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 25 pamoja na , na mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku anayetarajiwa kuchukua nafasi yake. ***(Calciomercato)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DE BRUYNE AWAANGUKIA MASHABIKI WA UBELGIJI

●●● Ni kutokana na timu yao kuzomewa baada ya kushindwa kupata...

**STUTTGART,** UJERUMANI

KEVIN de Bruyne aliwataka mashabiki wa Ubelgiji wenye hasira kuiunga mkono timu baada ya kuwaambia wachezaji wenzake waondoke uwanjani mwishoni mwa mchezo wa Kundi E dhidi ya Ukraine uliomalizika kwa suluhu na kusababisha kuzomewa mara kwa mara na mashabiki wa nchi hiyo waliosafiri na kikosi hicho.

Sare hiyo katika mechi iliyochezwa katika mji wa Stuttgart ilitosha kufuzu kwa hatua ya 16 bora kwa Ubelgiji na sasa watamenyana na Ufaransa keshokutwa huko Dusseldorf, huku ikishuhudiwa Ukraine ikiwa timu ya kwanza kuondolewa kwenye michuano ya Ulaya ikiwa na pointi nne.

Wakati Ubelgiji ikitinga hatua ya 16 bora, mashabiki walijibu kwa hasira mwishoni mwa mchezo kwa kuwazomea wachezaji.

De Bruyne alikaribia sehemu ya mashabiki wa Ubelgiji, lakini aligeuka nyuma na kuwaamuru wachezaji wenzake waondoke uwanjani huku kelele zikiongezeka wakati jina lake lilipotangazwa ni mchezaji bora wa mechi.

"Tulijaribu kushinda mechi," alisema De Bruyne katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Tulikuwa na nafasi za kufunga mabao, lakini hatukuweka hatari yoyote.

"Ikitokea hivyo, umetoka kwenye michuano ya Euro. Ni aibu hatukufanikiwa kufunga hapo awali -- tulipata nafasi -- na baada ya hapo tunahitaji tu mashabiki kusalia nasi.

"Tunawahitaji mashabiki hawa. Tutawahitaji dhidi ya Ufaransa. Hilo ndilo ninalopaswa kusema."

Alipoulizwa kwa nini aliwataka wachezaji wenzake kuondoka uwanjani na kutokaribia mashabiki wa Ubelgiji mwishoni, De Bruyne alitoa jibu lililolindwa kwa kukariri wito wa kuungwa mkono na mashabiki.

"Tunazihitaji tu," alisema. "Sijui niseme nini kingine. Tunawahitaji mashabiki tu. Tutawahitaji dhidi ya Ufaransa. Tuliwahitaji katika mechi tatu zilizopita. Ni hivyo."

Kocha wa Ubelgiji, Domenico Tedesco, aliunga mkono maoni ya De Bruyne kwa kusema wachezaji wake walikuwa wakijaribu kushinda mchezo huo katika hatua za mwisho.

# KIVUMBI 16 BORA EURO 2024



**BERLIN,** UJERUMANI

DROO ya hatua ya 16 bora ya mashindano ya Euro 2024 imekamilika baada ya mechi za mwisho za hatua ya makundi ya michuano hiyo kukamilika juzi usiku.

England itamenyana na Slovakia katika hatua hiyo mechi itakayochezwa kwenye Uwanja wa Arena AufSchalke wakati Hispania yenye kiwango bora itakipiga dhidi ya Georgia.

Mechi nyingine itakuwa ni kati ya Ufaransa dhidi ya Ubelgiji mchezo ambao unatarajia kuvutia hisia za watu wengi zaidi huku wenyeji Ujerumani iliyopita bila kupingwa hatua ya makundi mbele ya mashabiki wa nyumbani, sasa wana kibarua kizito kuwavaa Denmark ambao wanaweza kuwa hatari muda wowote.

Huenda tukashuhudia mechi bora zaidi ya Euro hii iwapo Ujerumani na Hispania zitakutana katika robo fainali kama zote zitavuka kihunzi cha hatua ya mtoano.

Ureno haitataka kuwazia kichapo chao cha mwisho cha hatua ya makundi dhidi ya Georgia wakati wakijiandaa kukabiliana na Slovenia.

Romania itakutana kwa mara ya kwanza na Uholanzi katika mtoano ya michuano hiyo ndani ya miaka 24 pale machinjioni Allianz Arena.

Huku Austria ya Kocha, Ralf Rangnick, itapepetana na Uturuki dimbani la Red Bull Area, Jijini Leipzig huku Uswizi wakikipiga na Italia.

Mechi zote 16 zitachezwa kwa muda wa siku nne kati ya Juni 29 hadu Julai 2, mwaka huu.

## Shaw fiti kuichezea England

**BERLIN,** UJERUMANI

MLINZI wa Timu ya Taifa ya England, Luke Shaw, ana imani atakuwa katika kikosi kitakachocheza dhidi ya Slovakia kwenye hatua ya ya mtoano wa 16 bora hapo keshokutwa.

Mlinzi huyo wa kushoto ana matumaini ya kujaribu kucheza katika mchezo huo muhimu baada ya kupona majeraha yake ya misuli ya paja ambayo yalimweka nje ya dimba katika michezo yote ya hatua ya makundi.

Shaw alirejea katika mazoezi rasmi na kikosi mapema wiki hii baada ya kuwa na mazoezi binafsi kitu ambacho kilizua hofu huenda asicheze hata mchezo mmoja kwenye mashindano hayo yanayofanyika Ujerumani. Alipoulizwa na waandishi wa habari ni lini anaweza kuwa tayari kujumuishwa kwenye mchezo wa Euro 2024 alijibu “mchezo ujao”. Kutokana na uwepo wa Kieran Trippier katika nafasi ya beki wa kushoto,huenda Shaw akaanzia benchi lakini huenda Gareth Southgate akampatia dakika kadhaa kutokana na umuhimu wake katika kikosi.

## Kvaratskhelia: Georgia imeweka historia Euro

**GELSENKIRCHEN,** UJERUMANI

NYOTA wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, amesema mkutano wa kabla ya mechi na Cristiano Ronaldo ulisaidia kuhamasisha imani timu yake inaweza kupata ushindi wa kihistoria dhidi ya Ureno na kufuzu kwa hatua ya 16 bora ya Euro 2024.

Georgia walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya washindi wa Euro 2016, Ureno kwenye Uwanja wa AufSchalke, huku Kvaratskhelia akifungua ukurasa wa mabao baada ya sekunde 92 na Georges Mikautadze, mfungaji bora wa michuano hiyo akifunga magoli matatu, akiongeza la pili kupitia penalti.

Ushindi huo utawafanya wakutane na Hispania huku Georgia wakifika hatua ya mtoano katika mechi yao ya kwanza ya michuano mikubwa, huku Kvaratskhelia akiondoka na jezi ya Ronaldo.

“Nimeipata jezi ya Ronaldo na tumefanikiwa kuingia katika raundi inayofuata,“ alisema Kvaratskhelia, ambaye alimtaja Ronaldo kama ndio kipenzi tangu utotoni kabla ya mchezo, katika mkutano na waandishi wa habari.

“Hii ni siku bora zaidi katika maisha ya mashabiki wa soka wa Georgia. Tumeweka historia, hakuna ambaye angeamini tungefanikisha.

„Hakuna ambaye angeamini tunaweza kuishinda Ureno lakini ndio maana sisi ni timu yenye nguvu, ikiwa kuna nafasi hata ya asilimia moja, tumeonyesha tunaweza kuifanya.

“Kabla ya mechi kulikuwa na mkutano ma Ronaldo na alinitakia mafanikio, sikuwahi kufikiria angekuja na kuzungumza nami.

“Ni mchezaji mzuri na mtu mzuri. Ndio maana ana utu mkubwa ndani na nje ya soka, namheshimu sana, ni mmoja wa wachezaji bora duniani.

“Anapokuja kuzungumza nawe kabla ya mechi, hiyo inashangaza, hiyo ilitusaidia kuamini tunaweza kufanya kitu leo (juzi).“

Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 23, ameonja mafanikio katika soka ya klabu, akishinda Serie A ya Italia na Napoli mnamo mwaka 2023, lakini amesema kuandika historia na nchi yake ilikuwa siku bora zaidi maishani mwake.

“Scudetto ilikuwa wakati wa kukumbukwa kwangu lakini nina furaha zaidi kwa sababu unapochezea nchi yako, inakupa furaha sana,“ aliongeza.

HABARI MICHEZO

# DUBE, AZAM WAMALIZANA RASMI, HURU KUTUA KOKOTE

**Na Somoe Ng'itu**

MSHAMBULIAJI wa Azam FC, Prince Dube, amelipa kiasi cha Dola za Marekani 200,000 kwa klabu hiyo ili kuvunja mkataba na kuanza mchakato wa kujiunga na timu nyingine, imefahamika.

Uongozi wa Azam ulimtaka mchezaji huyo au klabu inayomtaka kulipa kiasi cha Dola za Marekani 300,000 ili kuvunja mkataba uliokuwapo.

Lakini baada ya klabu hiyo ya Chamazi kutoa tamko hilo, pande hizo mbili zilikutana kufanya mazungumzo na hatimaye Dube alitakiwa kulipa kiasi hicho alichoweka benki ili kuwa mchezaji huru.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam jana, zinasema mshambuliaji huyo raia wa Zimbabwe alilipa kiasi hicho cha fedha tangu wiki iliyopita na sasa hivi Azam FC inasubiri kuona muamala huo umeingia kwenye akaunti yao.

Chanzo chetu kimesema uongozi wa Azam umethibitisha kupokea viambatanisho vya malipo hayo lakini wanasubiri kuzipokea rasmi ndani ya akaunti yao.

"Ni kweli Dube alifanya malipo ya Dola 200,000 na kuwasilisha karatasi halisi za malipo hayo kwa uongozi wa Azam, lakini kama unavyojua taratibu za fedha na kibenki, pesa hiyo bado kwetu haijasomeka.

Mara baada ya kuzipokea, tutaweka wazi kama ambavyo tulifanya wakati wa nyuma mchezaji wetu alipoonyesha nia ya kutaka kuondoka kwenda kujaribu changamoto mpya," kilisema chanzo chetu.

Habari zinasema Dube anatarajia kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na ndio waliofanikisha mchakato huo kumalizika mapema.

Klabu hiyo pia inatajwa kugharamia ziara ya mapumziko ya mshambuliaji huyo nchini Ufaransa.



Wachezaji wa Maendeleo Queens ya Songwe wakifurahi baada ya kuifunga TSC Queens ya Mwanza mabao 4-1 katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa wa Mikoa kwa Wanawake (WRCL 2024), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Fountain Gate jijini Dodoma jana. **PICHA: TFF**

# Twiga Stars kambini Julai

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuingia kambini Julai Mosi ili kujiandaa na mechi mbili za kirafiki za kimataifa, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF), Clifford Ndimbo, aliliambia gazeti hili jana, Twiga Stars itacheza mechi za kirafiki dhidi ya wenzao wa Tunisia na Botswana.

Ndimbo alisema mechi hizo zinalenga kukiimarisha kikosi hicho ambacho kimekata tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON), ambazo sasa zitafanyika Julai, mwakani nchini Morocco.

"Kikosi cha Twiga Stars kitakuwa na mechi mbili za kirafiki za kimataifa, watacheza dhidi ya Tunisia na Botswana, kitaingia kambini Julai Mosi chini ya Bakari Shime (Kocha Mkuu)," Ndimbo alisema. Aliwataja wachezaji waliotwa ni Najat Abasi wa JKT, Asha Mrisho (Amani), Lidya Maximilian (JKT), Protasia Mbunda (Fountain Gate), Enekia Kasonga (Eastern Flames), Julietha Singano, Violeth Mwamakamba (Simba), Joyce Lema, Anastazia Katunzi, Janeth Christopher (JKT), Esther Maseke (Bunda) na Diana Lucas kutoka Ame SFK.

Wachezaji wengine ni Aisha Mnunka (Simba), Stumai Athuman, Winifrida Gerald (JKT), Maimuna Kaimu- (ZD ya Misri), Elizabert Charles (Alliance), Aisha Masaka (Bk Hacken), Oppa Clement (Besiktas) na Clara Luvanga wa Al Nasir ya Saudi Arabia.

# Simba kushusha silaha tatu mpya

INATOKA UK. 24

kumaliza tatizo la kiungo mkabaji katika kikosi cha Simba.

„Huyu ana umbile kubwa, alivyo kama Khalid Aucho au Thadeo Lwanga, sehemu iliyokuwa inatusumbua sana Simba kwa muda mrefu ni ya kiungo mkabaji, huyu ni mmoja wa wanaokuja kuziba pengo, huku nyuma nilikwambia kuna mbadala wa Mohamed Hussein, anakuja, mambo yamekamilika, nadhani wiki hii Valentin atakuja kwa ajili ya vipimo vya afya na kusaini mkataba wa miaka mitatu, ni kijana mdogo ana miaka 23 tu," kiliongeza.

Wakati huo huo, habari zinasema winga msumbufu, Mutale, raia wa Zambia ameshawasili nchini akiwa na familia yake tayari kwa kusaini mkataba wa kuitumikia Simba.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amekiri wachezaji wapya watakaovaa jezi ya klabu hiyo katika msimu mpya watawasili wakati wowote kuanzia wikendi hii.

"Nilisema na nitaendelea kusema, safari hii hatufanyi mzaha, tunafanya usajili mkubwa, na tutaachana na wachezaji wengi watapewa ‚thank you', wapo tutakaoachana nao kwa kumaliza mikataba na wengine tutaivunja, lengo ni kupata wachezaji wenye viwango bora," Ahmed alisema.

# Sekilojo ashauri mambo 4 Yanga

INATOKA UK. 24

Diarra, kipindi hiki ambacho Metacha Mnata ameondoka ndani ya timu hiyo.

"Sijajua Yanga wamefikia wapi na Mshery (Abdultwalib), kwa sababu nimesikia amemaliza mkataba, lakini bado kuna haja ya kuongeza kipa mwingine kwa ajili ya kumsaidia Diarra," alisema nyota huyo.

Aliongeza wapo wachezaji ambao wataachwa na timu hiyo kwa kufuata uamuzi wa Gamondi, hivyo viongozi watumie nafasi hizo kuongeza wachezaji watakaokuwa na mchango mkubwa kwa timu.

Habari zilizopatikana jijini kutoka ndani ya Yanga zinasema Sowah ambaye kwa sasa anaitumikia Al Nasr Benghazi ya Libya anakuja kuchukua nafasi ya Joseph Guede ambaye huenda akaondoka ndani ya kikosi hicho kilichoko chini ya Kocha Mkuu, Miguel Gamondi.

Chanzo hicho kiliendelea kusema mazungumzo kati ya Yanga na mchezaji huyo yamemalizika na sasa wameanza mchakato wa kumalizana na klabu yake kwa sababu bado ana mkataba.

"Viongozi wameonekana wanamhitaji, hasa baada ya yeye kutokuwa na furaha na timu hiyo (Al Nasr), alijiunga nayo Januari, mwaka huu lakini anataka kuondoka, uzuri mchezaji mwenyewe amekuwa na mahusiano mazuri na uongozi wetu baada ya kufahamiana tulipocheza mechi mbili za mashindano Ligi ya Mabingwa Afrika, na ilikuwa kidogo asajiliwe kipindi cha dirisha dogo, lakini ikashindikana akaenda Libya," kilisema chanzo hicho.

Medeama ilikuwa Kundi D pamoja ya Yanga katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliomalizika na mchezaji huyo alionekana akiisumbua safu ya ulinzi ya Gamondi katika mechi zote mbili, akifunga bao la penalti katika mchezo wa kwanza uliyochezwa Desemba 8, mwaka jana huko Ghana, timu hizo zikitoka sare ya goli 1-1, na alikosa tuta katika mechi ya pili iliyochezwa nchini, baada ya wiki mbili, wenyeji wakishinda mabao 3-0.

Chanzo kingine kilisema Yanga iko katika mipango ya kumsajili kiungo mkabaji chipukizi, Mtasigwa, ambaye amepata makuzi mazuri ya soka lake nchini Iceland na kabla ya kujiunga na Azam msimu wa 2023/2024.

"Alituvutia sana hasa kwenye mechi anazocheza katika kikosi cha Stars, na ‚tulimvulia kofia' kiwango alichoonyesha katika mchezo wa fainali ya Kombe la FA pale New Amaan Complex (Zanzibar) ingawa Yanga ilitwaa ubingwa," kiliongeza chanzo chetu.

Yanga pia inatajwa inahitaji kumsajili kiungo mkabaji wa Azam FC na Taifa Stars, Adolf Mtasigwa.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema jana hawawezi kuzungumza lolote kuhusu usajili kwa sababu bado wako mapumzikoni baada ya kazi ngumu ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, Kombe la FA na kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Jamani tuacheni kwanza tule bata, kazi ilikuwa ngumu, kwa sasa tupo mapumzikoni, subirini kuanzia Julai Mosi kila kitu tutaanza kukiweka hadharani," alisema Kamwe.

Hatimaye Yanga imeondolewa kifungo cha kusajili baada ya kumalizana na aliyekuwa mchezaji wao, Lazaraus kambole, Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), limesema jana katika taarifa yake.

Yanga sasa pia itakuwa huru kufanya usajili wa ndani.

Michezo
Ijumaa Juni 28, 2024

De Bruyne awaangukia mashabiki wa Ubelgiji

UKURASA 21



# Sekilojo ashauri mambo 4 Yanga

**Mkongwe huyo anaamini ikifanya hivyo itakuwa tishio, Mghana Sowah anukia...**

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikiwa katika dakika za mwisho za kumnasa mshambuliaji wa zamani wa Medeama FC ya Ghana, Jonathan Sowah, aliyekuwa mchezaji nyota wa timu hiyo na Taifa Stars, Sekilojo Chambua, ameanika mambo manne muhimu ambayo mabingwa hao wanatakiwa kufanya ili kuwa na kikosi tishio kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Chambua alisema ili Yanga iendeleze makali yake katika mashindano ya ndani na ya kimataifa watakayoshiriki msimu ujao, inatakiwa kuboreshwa kwenye eneo la beki wa kati, eneo la mshambuliaji wa kati na winga.

Chambua alisema kama Yanga itaongeza nguvu katika maeneo hayo, anaamini itakuwa na nafasi ya kufika mbali kwenye mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Kocha wetu Gamondi yeye anafahamu zaidi nini cha kufanya kukiongezea ubora kikosi chetu, lakini mimi nadhani tunapaswa kuongeza mshambuliaji mmoja wa kati mwenye uwezo mkubwa, winga mwenye damu changa lakini uwezo mkubwa pamoja na beki mmoja wa kati kwa ajili ya kuja kuwasaidia Dickson Job na Bacca (Ibrahim Hamad)," alisema Sekilojo.

Alisema Yanga pia wanapaswa kutafuta golikipa mwingine kwa ajili ya kumsaidia Djigui

INAENDELEA UK. 23



Mchezaji nyota wa Timu ya Taifa ya Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, akishangilia baada ya kufunga bao la kwanza katika mechi ya Kundi D ya michuano ya Euro 2024 dhidi ya Ureno iliyochezwa juzi usiku. Georgia ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# Simba kushusha silaha tatu mpya

**Na Adam Fungamwango**

WEKUNDU wa Msimbazi wako katika hatua za mwisho za kuwasajili nyota wapya watatu ambao wanatarajiwa kuwasili nchini wakati wowote ili kukamilisha taratibu za kujiunga na Simba, ikiwamo kufanya vipimo vya afya.

Wachezaji hao ambao wanatajwa kukaribia kujiunga na Simba ni pamoja na kiungo mshambuliaji, Jean Charles Ohoua, mwenye umri wa miaka 22 kutoka Stella Adjame ya Ivory Coast, kiungo mkabaji, Debora Mavambo, ambaye anaichezea Mutondo Stars ya Zambia na beki wa kushoto, Valentin Nouma kutoka Rahimo FC.

Taarifa zilizopatikana kutoka ndani ya Simba zinasema wachezaji hao walishafikia makubaliano ya awali na kilichobakia ni kukamilisha taratibu za mwisho baada ya kutua nchini.

Kiliongeza pia nyota wote wapya waliosajiliwa na Simba wanatakiwa kuwasili Dar es Salaam Julai Mosi ili kuendelea na maandalizi ya safari ya kuelekea Morocco ambapo wanaenda kuweka kambi kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya.

Kilisema pia nyota hao watapiga picha rasmi zitakazotumika katika zoezi la utambulisho.

"Ohoua ndiye mchezaji bora wa msimu wa 2023/2024 nchini Ivory Coast, anacheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, amehusika na mabao 21 (amefunga magoli 12 na asisti tisa), sasa nikwambie tu huyu mchezaji amesajiliwa rasmi kuchukua mikoba ya Clatous Chama, huyu ndiye atauzika ufalme wake, viongozi wamefikia uamuzi wa kuleta ,mashine' mpya kwa sababu jamaa (Chama), umri umekwenda halafu amekuwa msumbufu, ili tumfanye atulie ni kumletea mtu kama yeye au zaidi yake," kilisema chanzo hicho kutoka Msimbazi.

Chanzo hicho kiliongeza, Mavambo ambaye anacheza Ligi Kuu Zambia anatajwa kuwa ni mmoja wa wachezaji wanaotarajiwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >